

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

**MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI
YA SERIKALI KWA MWAKA 2023/24**

DESEMBA, 2022

**KAULI YA KATIBU MKUU HAZINA NA MLIPAJI MKUU WA SERIKALI
KUHUSU MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI YA
SERIKALI KWA MWAKA 2023/24**

Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2023/24 umeandaliwa kwa mujibu wa Sheria ya Bajeti, Sura 439 na Kanuni zake za mwaka 2015. Mwongozo umeainisha masuala ya kuzingatiwa na Maafisa Masuuli wote wa Wizara, Idara zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mashirika na Taasisi za Umma wakati wa maandalizi, utekelezaji, ufuatiliaji tathmini na utoaji wa taarifa za mpango na bajeti.

Maafisa Masuuli mnasisitizwa kuandaa mipango na bajeti zenu za mwaka 2023/24 kwa umakini mkubwa kwa kuzingatia wigo wa ukomo wa bajeti utakaotolewa kwa kila Fungu, maelekezo ya Mwongozo na vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/24. Aidha, ili kuwianisha mapato na matumizi, mnasisitizwa kuelekeza fedha kwenye maeneo ya vipaumbele vya kisekta na majukumu ya msingi ya Taasisi zenu kwa mujibu wa "Instrument", kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika shughuli za Serikali na kuzingatia Waraka wa Mkuu wa Utumishi wa Umma Na. 2 wa Mwaka 2021 kuhusu utaratibu wa kutumia magari, aina na stahili za Magari kwa viongozi katika utumishi wa Umma.

Katika kusimamia dhana ya uwajibikaji na uwazi katika utendaji kazi, mnatakiwa kuimarisha vitengo vya Ukaguzi wa Ndani kwa kuvipatia vitendea kazi na kuhakikisha vina watumishi wa kutosha, kutumia matokeo ya taarifa za Mdhambi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuleta mabadiliko chanya katika utendaji kazi, kudhibiti uzalishaji wa madeni na kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Kuthibiti na Kuzuia Malimbikizo ya Madeni ulioboreshwa wa mwaka 2022.

Nimatarajio yangu kuwa mtazingatia matakwa ya Sheria ya Bajeti, SURA 439; Sheria ya Fedha za Umma, SURA 348, Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 na Miongozo ya Serikali katika kufanikisha utekelezaji wa vipaumbele vya Serikali kwa tija na ufanisi ili kutoa huduma bora kwa wananchi. Utekelezaji wa Mipango na Bajeti zenu kwa tija na ufanisi utaimarisha usimamizi wa matumizi ya fedha za umma; utawala bora unaozingatia misingi ya sheria; kuongeza ushiriki wa wadau katika uandaaji, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya Mpango na Bajeti na hatimaye kuchochea ukuaji wa uchumi na kuongeza upatikanaji wa huduma za jamii.

Ninawatakia utekelezaji mwema.



Emmanuel M. Tutuba

**KATIBU MKUU HAZINA NA
MLIPAJI MKUU WA SERIKALI**

YALIYOMO

MUHTASARI.....	vii
SEHEMU YA KWANZA	x
SERA NA MFUMO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24.....	x
SURA YA KWANZA.....	1
MAPITIO YA MWENENDO NA MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI.....	1
1.1 Utangulizi	1
1.2 Mwenendo na Mwelekeo wa Uchumi wa Dunia na Kikanda.....	1
1.3 Mwenendo na Mwelekeo wa Mfumuko wa Bei wa Dunia na Kanda.....	3
1.4 Mwenendo na Mwelekeo wa Uchumi wa Tanzania.....	4
1.5 Deni la Serikali	10
SURA YA PILI	12
MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2021/22	12
2.1 Utangulizi	12
2.2 Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2021/22	12
2.2.1 Mapato na Matumizi.....	13
2.3 Mafanikio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti.....	14
2.3.1 Mafanikio katika Utekelezaji wa Miradi ya Kielelezo na Kimkakati	15
2.3.2 Changamoto zilizojitokeza Katika Utekelezaji wa Bajeti	15
2.3.3 Hatua Zilizochukuliwa Kukabiliana na Changamoto	16
SURA YA TATU.....	17
MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2022/23	17
3.1 Utangulizi	17
3.2 Muundo wa Bajeti ya Mwaka 2022/23	17
3.3 Mwenendo wa Utekelezaji wa Bajeti kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2022/23	18
3.3.1 Mapato	18
3.3.2 Matumizi.....	19
3.4 Utekelezaji wa Maelekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2022/23	19
SURA YA NNE.....	24
MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2023/24.....	24
4.1 Utangulizi	24
4.2 Malengo na Shabaha ya Uchumi Jumla	24
4.3 Misingi ya Uchumi Jumla.....	24
4.4 Vipambe katika mwaka 2023/24	24
4.5 Mfumo wa Makadirio ya Mapato na Matumizi wa mwaka 2023/24.....	25
4.6 Sera za Mapato na Makadirio katika Muda wa Kati.....	25
4.7 Sera za Misaada na Makadirio katika Muda wa Kati	27

4.7.1 Sera za Misaada	27
4.8 Sera za Matumizi na Makadirio katika Muda wa Kati	28
4.8.1 Mikakati ya Kusimamia Matumizi	28
4.8.2 Makadirio ya Matumizi	29
4.8.3 Makadirio ya Matumizi Kisekta	31
4.9 Ugharamiaji wa Nakisi ya Bajeti	32
4.10 Sura ya Bajeti	33
SURA YA TANO.....	39
VIHATARISHI VYA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI PAMOJA NA MIKAKATI YA KUKABILIANA NAVYO	39
5.1 Utangulizi	39
5.2 Vihatarishi vya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali	39
5.3 Athari za vihatarishi katika utekelezaji wa mpango na bajeti.....	39
5.4 Hatua za kukabiliana na vihatarishi.....	40
SEHEMU YA PILI.....	42
MAELEKEZO YA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24	42
SURA YA KWANZA.....	43
MAELEKEZO YA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2023/24	43
1.1. Utangulizi	43
1.2. Uandaaji wa Mpango na Bajeti.....	43
1.3. Kamati za Bajeti	43
1.4. Ukusanyaji wa Mapato	43
1.5. Kiwango cha Ubadilishaji Fedha.....	45
1.6. Maandalizi ya Bajeti ya Mishahara	45
1.7. Maandalizi ya Bajeti ya uendeshaji wa Ofisi.....	46
1.8. Maandalizi na Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo	46
1.9. Masuala Mengine ya Kuzingatiwa katika Uandaaji wa Mpango na Bajeti	48
1.10. Masuala Mtambuka katika Mpango na Bajeti.....	52
1.11. Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa	53
1.12. Maelekezo Mahsusi kwa Taasisi na Mashirika ya Umma.....	53
1.13. Maelekezo kwa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa	54
1.13.1. Sekretarieti za Mikoa.....	54
1.13.2. Mamlaka za Serikali za Mitaa	55
1.14. Uingizaji wa Takwimu za Bajeti ya Serikali kwenye Mifumo ya CBMS na PlanRep.....	58
1.15. Uwasilishaji na Uchambuzi wa Mpango na Bajeti	58
1.16. Uwasilishaji wa Randama	59
1.17. Ufuatiliaji, Tathmini na Utoaji wa Taarifa za Utekelezaji.....	59

1.17.1.	Ufuatiliaji na Tathmini.....	59
1.17.2.	Uwasilishaji wa Taarifa za Utekelezaji.....	60
SURA YA PILI		61
MUUNDO WA UANDAAJI NA UWASILISHAJI WA TAARIFA ZA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2023/24		61
2.1	Utangulizi	61
2.2	Maandalizi ya Mpango na Bajeti.....	61
2.3	Mpangokazi na Mtiririko wa Mahitaji ya Fedha	62
2.4	Taarifa za Utekelezaji wa Mpango na Bajeti.....	62

ORODHA YA VIFUPISHO

ASDP	Agriculture Sector Development Programme
APF	Alternative Project Financing
CBMS	Centralized Budget and Management System
CCM	Chama Cha Mapinduzi
CFR	Council Financial Report
CFS	Consolidated Fund Service
DCF	Development Co-operation Framework
DEV	Development
EAC	East African Community
EACOP	East African Crude Oil Pipeline
EPC+F	Engineering Procurement Construction and Financing
FFARS	Facility Financial Accounting and Reporting System
FY	Financial Year
FYDP	Five Year Development Plan
GPSA	Government Procurement Services Agency
GAMIS	Government Asset Management Information System
GePG	Government Electronic Payment Gateway
GFS	Government Finance Statistics
HCMIS	Human Capital Management Information System
IMF	International Monetary Fund
LGAs	Local Government Authorities
LNG	Liquefied Natural Gas
M3	Extended Broad Money Supply
MDAs	Ministries, Independent Departments and Agencies
MTEF	Medium Term Expenditure Framework
MTSPBM	Medium Term Strategic Plan and Budget Manual
MUSE	Mfumo wa Ulipaji Serikalini
MW	Megawatts
NHIF	National Health Insurance Fund
NPMIS	National Project Management Information System
OC	Other Charges
OR-MUUB	Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora
OR-TAMISEMI	Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
OTRMIS	Office of Treasury Registrar Management Information System
PE	Personal Emoluments
PlanRep	Planning and Reporting Database
PPP	Public-Private-Partnership
PSRP	Public Sector Reform Program
PSSSF	Public Service Social Security Fund
RSs	Regional Secretariats

SADC	Southern Africa Development Community
SDG	Sustainable Development Goals
SGR	Standard Gauge Railway
TARURA	Tanzania Rural and Urban Roads Agency
TANePS	Tanzania National e-Procurement System
TASAF	Tanzania Social Action Fund
TEHAMA	Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
TeSWs	Tanzania Electronic Single Window System
UKIMWI	Upungufu wa Kinga Mwilini
UVIKO - 19	Ugonjwa wa Virusi vya Korona
VAT	Value Added Tax
VVU	Virusi Vya Ukimwi
WCF	Workers Compensation Fund
ZSSF	Zanzibar Social Security Fund

MUHTASARI

Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2023/24 umeandaliwa kwa mujibu wa Sheria ya Bajeti, Sura 439 na Kanuni zake za mwaka 2015. Uandaaji wa Mwongozo huu umefanyika kwa kurejea vipaumbele vilivyoainishwa kwenye dira, sera, mikakati na miongozo ya maendeleo kitaifa na kimataifa. Nyaraka zilizorejewa ni pamoja na: Mpango wa Maendeleo wa Taifa (2021/22 – 2025/26); Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; Mpango Kazi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara; Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha (2020/21 -2029/30); Sheria ya Bajeti, Sura 439; Sheria ya Madeni, Dhamana na Misaada, Sura 134; Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348; Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410; Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu; Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo; Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030; Agenda ya Afrika Mashariki 2050; Dira ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika 2050; na Agenda ya Afrika 2063.

Lengo la Mwongozo wa Mpango na Bajeti ni kuelekeza namna bora ya ukusanyaji wa mapato na utengaji wa raslimali fedha za kutekeleza Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa mwaka 2023/24 ili kufikia mafanikio ya kijamii na kiuchumi. Pia, Mwongozo huu unalenga kutoa maelekezo kwa Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali; Sekretarieti za Mikoa; Mamlaka za Serikali za Mitaa; Taasisi na Mashirika ya Umma kuzingatia vipaumbele vya kitaifa na kisekta wakati wa maandalizi ya mipango na bajeti.

Mwongozo umegawanyika katika sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza ni Sera na Mfumo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2023/24 ambayo inajumuisha: Mapitio ya Mwenendo na Mwelekeo wa Hali ya Uchumi; Mapitio ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2021/22; mapitio ya utekelezaji wa Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2022/23; Mpango na Bajeti kwa mwaka 2023/24 ambao unaainisha makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2023/24 na muda wa kati pamoja na sera na mikakati ya kusimamia mapato na matumizi; na uchambuzi wa vihatarishi vya utekelezaji wa mpango na bajeti, ukuaji wa uchumi na mikakati ya kukabiliana navyo. Sehemu ya pili inatoa maelekezo ya kuzingatiwa na Maafisa Masuuli katika uandaaji, uwasilishaji na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2023/24.

Katika mwaka 2021, uchumi wa Tanzania ulikua kwa asilimia 4.9 ikilinganishwa na matarajio ya asilimia 5.0 na ukuaji halisi wa asilimia 4.8 mwaka 2020. Sekta zilizokuwa na viwango vikubwa vya ukuaji ni pamoja na: shughuli za burudani na sanaa (asilimia 19.4) ikifuatiwa na umeme (asilimia 10.0), madini (asilimia 9.6) na habari na mawasiliano (asilimia 9.6). Kuimarika kwa kasi ya ukuaji wa uchumi kulitokana na: utekelezaji wa Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020

pamoja na uwekezaji uliofanywa na Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hususan katika miundombinu ya afya, elimu, nishati, maji, ujenzi; shughuli za kiuchumi zilizotokana na ongezeko la mikopo katika sekta binafsi; uchimbaji wa madini; na utawala bora unaozingatia misingi ya sheria

Katika mwaka 2022, uchumi unatarajiwa kukua kwa asilimia 4.7 ukiakisi changamoto zinazoukumba uchumi wa dunia ikiwemo vita inayoendelea nchini Ukraine. Hata hivyo, makadirio haya ni zaidi ya wastani wa ukuaji wa nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara wa asilimia 3.8 mwaka 2022. Kwa mwaka 2023 ukuaji wa uchumi unatarajiwa kuanza kuongezeka kufikia makadirio ya asilimia 5.3. Maoteo ya ukuaji wa uchumi wa Tanzania yamezingatia hatua zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi kukabiliana na athari zitokanazo na vita inayoendelea nchini Ukraine ikiwemo uimarishaji wa sekta za uzalishaji na huduma za jamii; utekelezaji wa miradi inayochachua shughuli za uchumi; na uboreshaji wa mazingira ya biashara na uwekezaji.

Katika mwaka 2021/22, Serikali imekusanya shilingi bilioni 36,924.8 sawa na asilimia 97 ya lengo la shilingi bilioni 37,992.5 ambapo shilingi bilioni 24,395.6 ni mapato ya ndani; na shilingi bilioni 12,529.2 ni misaada na mikopo ya ndani na nje ya nchi. Aidha, Serikali ilitumia shilingi bilioni 37,251.8 kugharamia shughuli mbalimbali za maendeleo na kawaida. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 22,561.5 ni matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 14,654.3 ni matumizi ya maendeleo.

Mapitio ya utekelezaji wa Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2022/23 yameonesha kuwa Bajeti ya Serikali iliyoidhinishwa na Bunge ilikuwa shilingi bilioni 41,480.6 sawa na ongezeko la shilingi bilioni 2,093.6 kutoka makadirio ya shilingi bilioni 39,387.0 yaliyopendekezwa katika Mwongozo.

Utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2022/23 kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2022/23, Serikali imekusanya mapato ya ndani yenye jumla ya shilingi bilioni 9,181.8 sawa na asilimia 93.2 ya lengo la shilingi bilioni 9,848.9. Aidha, katika kipindi hicho Serikali imetoa ridhaa ya matumizi ya shilingi bilioni 9,153.8 sawa na asilimia 92.9 ya lengo la shilingi bilioni 9,848.9.

Mapato ya ndani yakijumuisha mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa yanakadiriwa kuongezeka hadi shilingi bilioni 31,034.6 mwaka 2023/24 kutoka makadirio ya shilingi bilioni 28,017.9 mwaka 2022/23. Katika kipindi cha muda wa kati, mapato yanakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 10.3 na kufikia shilingi bilioni 37,642.9 mwaka 2025/26. Mchango wa mapato ya ndani katika bajeti unakadiriwa kuongezeka kutoka asilimia 67.5 mwaka 2022/23 hadi asilimia 72.9

mwaka 2023/24 na kuongezeka hadi asilimia 76.3 mwaka 2025/26. Mapato ya ndani kwa Pato la Taifa yanakadiriwa kuwa wastani wa asilimia 15.2 katika muda wa kati.

Katika kipindi hicho, matumizi ya Serikali yanakadiriwa kuongezeka hadi shilingi bilioni 43,294.6 sawa na asilimia 20.7 ya Pato la Taifa, kutoka makadirio ya shilingi bilioni 41,480.6 mwaka 2020/21. Katika muda wa kati, matumizi ya Serikali yanakadiriwa kuongezeka kwa wastani wa asilimia 8.4 kwa mwaka hadi shilingi bilioni 50,154.2 mwaka 2025/26.

Aidha, Serikali itaweka msukumo katika kutekeleza vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26) kwa kipindi muda wa kati. Katika mwaka 2023/24, maeneo yatakayopewa kipaumbele ni pamoja na kugharamia: miradi ya kielelezo inayoendelea; deni la Serikali; mishahara ya watumishi wa Umma; na huduma za jamii zikiwemo afya, elimu na maji. Vile vile, Serikali itaendelea kuimarisha sekta za uzalishaji na kuongeza kasi ya kufufua uchumi ulioathiriwa na UVIKO - 19, vita inayoendelea nchini Ukraine na mabadiliko ya tabianchi.

Kwa kutambua kwamba, utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2023/24 unaweza kuathiriwa na vihatarishi mbalimbali ikiwemo vinavyo athiri ukuaji wa uchumi jumla, Mwongozo umeainisha hatua zinazoweza kuchukuliwa ili kuepuka au kupunguza athari za vihatarishi hivyo katika kufikia shabaha za vipaumbele vya Taifa.

Mwongozo umeainisha masuala ya kuzingatiwa na Maafisa Masuuli wakati wa uandaaji, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini pamoja na utoaji wa taarifa. Baadhi ya maelekezo hayo ni pamoja na: kuhakikisha Kamati za Bajeti za Mafungu zinafanya kazi kwa kuzingatia matakwa ya Kifungu cha 18(2) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439 na Kanuni zake; kutenga bajeti kwa ajili ya matumizi yasiyoepukika hususan miradi inayoendelea, gharama za pango, umeme, simu, maji, ulinzi na usafi; kutenga bajeti ya kulipa madeni yaliyohakikiwa; kutenga bajeti kwa ajili ya kugharamia majukumu ya msingi ya Mafungu husika. Hivyo maombi nje ya bajeti hayatafanyiwa kazi; kutoajiri watumishi wapya hadi kuthibitisha upungufu uliopo na iwapo kuna waliozidi wahamishiwe sehemu zenye upungufu ili kuhakikisha uwepo wa msawazo wa watumishi (Manning Level); na kuzingatia Waraka wa Mkuu wa Utumishi wa Umma Na.2 wa mwaka 2021 kuhusu utaratibu wa kutumia magari, aina na stahili za magari kwa viongozi katika utumishi wa umma na hii ijitokeze kwenye bajeti ya mafungu husika. Watumishi waliofikia stahiki ya kuendeshwa kwa magari ya Serikali wakopeshwe magari na siyo kununuliwa na Serikali.

SEHEMU YA KWANZA

SERA NA MFUMO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24

SURA YA KWANZA
MAPITIO YA MWENENDO NA MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI

1.1 Utangulizi

1. Sura hii inaelezea mwenendo wa hali ya uchumi wa Tanzania, kikanda na dunia kwa mwaka 2021, pamoja na mwelekeo kwa kipindi cha mwaka 2022 hadi 2025. Aidha, sura hii inaelezea mwenendo wa viashiria vya uchumi wa Tanzania katika kipindi cha mwaka ulioishia Juni, 2022. Kwa ujumla, mwenendo wa uchumi katika kipindi cha mwaka 2021 ulianza kuimarika kutoka kwenye hali ya mdororo katika kipindi cha mwaka 2020 uliosababishwa na athari za UVIKO - 19. Hata hivyo, mwenendo wa uchumi ulianza kuyumba tena mwaka 2022 kufuatia athari ya vita inayoendelea kati ya nchi za Urusi na Ukraine pamoja na maambukizi mapya ya UVIKO - 19.

1.2 Mwenendo na Mwelekeo wa Uchumi wa Dunia na Kikanda

2. Uchumi wa dunia uliendelea kuimarika katika nusu ya pili ya mwaka 2021. Aidha, pamoja na kuimarika kwa uchumi wa dunia, kasi ya ukuaji imeanza kuathirika kutokana na: kuongezeka kwa bei za bidhaa katika soko la dunia; uwepo wa vita kati ya nchi za Urusi na Ukraine; na kuibuka kwa aina mpya ya virusi vya UVIKO-19 nchini China. Kwa mujibu wa Taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (International Monetary Fund - IMF) toleo la Julai 2022, uchumi wa dunia ulikua kwa asilimia 6.1 mwaka 2021 ikilinganishwa na ukuaji hasi wa asilimia 3.1 mwaka 2020. Kuimarika kwa uchumi wa dunia kwa mwaka 2021 kulisababishwa na utekelezaji wa sera madhubuti za fedha na bajeti zilizochochua kukua kwa shughuli za kiuchumi pamoja na kuendelea kuimarishwa kwa huduma za afya ikiwemo utoaji wa chanjo kwa lengo la kupunguza maambukizi ya UVIKO-19. Hata hivyo, uchumi wa dunia unatarajiwa kukua kwa kasi ndogo ya asilimia 3.2 mwaka 2022 na asilimia 2.9 mwaka 2023. Hali hii inatokana na changamoto zinazoikumba dunia na hatua za sera za fedha katika kupunguza athari za mfumuko wa bei zilizochukuliwa na Marekani na mataifa ya Ulaya yenye uchumi mkubwa.

3. Katika mwaka 2021 uchumi wa nchi zilizoendelea na nchi zinazoendelea ulikua kwa asilimia 5.2 na asilimia 6.8 ikilinganishwa na ukuaji hasi wa asilimia 4.5 na asilimia hasi 2.0 mwaka 2020, mtawalia. Ukuaji wa uchumi wa nchi zilizoendelea unakadiriwa kuwa asilimia 2.5 mwaka 2022 na asilimia 1.4 mwaka 2023. Kupungua kwa ukuaji wa uchumi kunatokana na sera ya fedha ya kupunguza ukwasi pamoja na athari hasi inayotokana na vita kati ya nchi za Urusi na Ukraine.

4. Ukuaji wa uchumi kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara ulikuwa asilimia 4.6 mwaka 2021 ikilinganishwa na ukuaji hasi wa asilimia 1.6 mwaka 2020. Hii ni kutokana na utulivu wa bei ya chakula na nishati pamoja na maboresho ya kisera kwa ajili ya kukabiliana na athari za UVIKO-19. Hata hivyo, kutokana na

athari ya vita kati ya nchi za Urusi na Ukraine, kasi ya ukuaji wa uchumi kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara inakadiriwa kupungua kufikia asilimia 3.8 mwaka 2022 na kuanza kuongezeka tena hadi asilimia 4.0 mwaka 2023. Mwenendo wa ukuaji wa uchumi wa dunia na kikanda ni kama unavyoonekana katika **Jedwali Na. 1.1.**

Jedwali Na. 1.1: Ukuaji wa Uchumi wa Dunia na Kikanda (Asilimia)

	Halisi		Maoteo	
	2020	2021	2022	2023
Dunia	-3.1	6.1	3.2	2.9
Nchi Zilizoundelea	-4.5	5.2	2.5	1.4
Nchi Zinazoendelea na Kuibukia Kiuchumi	-2.0	6.8	3.6	3.9
China	2.2	8.1	3.3	4.6
India*	6.6	8.7	7.4	6.1
Nchi za Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara	-1.6	4.6	3.8	4.0

Chanzo: Taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa Mwenendo na Mwelekeo wa Uchumi wa Dunia Toleo la Julai, 2022 (IMF-WEO Julai,2022)

*Kwa nchi ya India, Takwimu na maoteo ni kwa mwaka wa fedha

5. Mwenendo wa uchumi katika nchi za ukanda wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) umeendelea kuimarika kutoka kwenye athari za mlipuko wa UVIKO-19, ambapo kasi ya ukuaji wa uchumi kwa mwaka 2021 ulikuwa chanya kwa nchi zote ikilinganishwa na ukuaji hasi kwa nchi nyingi za kanda hizi. **Jedwali Na. 1.2** linaonesha mwenendo wa ukuaji wa uchumi kwa nchi za EAC na SADC.

Jedwali Na. 1.2: Ukuaji wa Uchumi kwa Ukanda wa Nchi Wanachama wa Afrika Mashariki na Uchumi Kusini mwa Jangwa la Sahara

Ukuaji wa Uchumi kwa nchi za SADC			
Nchi	2019	2020	2021
Angola	-0.7	-5.6	0.7
Botswana	3.0	-8.7	12.5
Comoros	1.8	-0.3	2.2
Tanzania	7.0	4.8	4.9
DRC	4.4	1.7	5.7
Eswatin	2.6	-1.9	3.1
Lesotho	0.0	-6	2.1
Madagascar	4.4	-7.1	3.5
Malawi	5.4	0.9	2.2
Mauritius	3.0	-14.9	3.9
Msumbiji	2.3	-1.2	2.2
Namibia	-0.9	-8.5	0.9
Seychelles	3.1	-7.7	8
Zambia	1.4	-2.8	4.3
Zimbabwe	-6.1	-5.3	6.3
Afrika ya Kusini	0.1	-6.4	4.9
Wastani	2.5	-4.3	4.2

Ukuaji wa Uchumi kwa Nchi za EAC			
Burundi	1.8	0.3	2.4
Kenya	4.9	-0.3	7.2
Rwanda	9.5	-3.4	10.2
Sudani Kusini	0.9	-6.6	5.3
Tanzania	7.0	4.8	4.9
Uganda	7.7	-1.4	5.1
Wastani	5.3	-1.1	5.9

Chanzo: Taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa Mwenendo na Mwelekeo wa Uchumi wa Dunia Toleo la Julai, 2022 (IMF-WEO Julai,2022).

1.3 Mwenendo na Mwelekeo wa Mfumuko wa Bei wa Dunia na Kanda

6. Mfumuko wa bei uliongezeka katika nchi nyingi duniani kutokana na mikwamo kwenye minyororo ya ugavi iliyotokana na athari za vita kati ya nchi za Urusi na Ukraine, pamoja na ongezeko la mahitaji. Kwa mujibu wa taarifa ya IMF ya mwezi Julai 2022 mfumuko wa bei wa dunia kwa mwaka 2021 uliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 4.7, ikilinganishwa na asilimia 3.2 mwaka 2020. Kwa mujibu wa taarifa hiyo, mfumuko wa bei kwa mwaka 2022 unatarajiwa kuendelea kuwa juu kufikia wastani wa asilimia 8.3 kutokana na kuvurugika kwa mnyororo wa ugavi uliochangia kuongezeka kwa bei za vyakula na mafuta katika soko la dunia. Aidha, katika nchi zinazoendelea mfumuko wa bei unatarajiwa kufikia asilimia 10.0 katika robo ya nne ya mwaka 2022.

7. Mfumuko wa bei katika nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliongezeka kufikia wastani wa asilimia 6.2 mwaka 2021/22 kutoka asilimia 4.5 mwaka 2020/21. Pamoja na ongezeko hili, mfumuko wa bei uliendelea kubaki ndani ya lengo la nchi wanachama wa EAC la chini ya asilimia 8. Ongezeko la kasi ya mfumuko wa bei lilichangiwa zaidi na ongezeko la bei za baadhi ya bidhaa zikiwemo vyakula, petroli, na mafuta ya kupikia (**Jedwali Na. 1.3**)

Jedwali Na. 1.3: Mfumuko wa Bei katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki

Nchi	Mfumuko wa Bei (Asilimia)	
	2020/21	2021/22
Tanzania	3.3	4.0
Uganda	2.5	3.4
Kenya	5.3	6.3
Rwanda	4.2	4.6
Burundi	7.1	12.5
Sudani ya Kusini	NA	NA
Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo	NA	NA
Wastani kwa Afrika Mashariki*	4.5	6.2

Chanzo: Ofisi za Taifa za Takwimu za Nchi Husika

NA: Hakuna takwimu


* Wastani kwa Afrika Mashariki bila kujumuisha nchi ya Sudani ya Kusini na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo mwaka 2020/21, 2021/22

1.4 Mwenendo na Mwelekeo wa Uchumi wa Tanzania

1.4.1 Mwenendo wa Pato la Taifa

8. Uchumi wa Tanzania umeendelea kuimarika kutokana na kufunguka kwa uchumi wa dunia na hatua zilizochukuliwa kufufua shughuli za kiuchumi ikiwemo hatua za kukabiliana na athari za UVIKO-19. Katika mwaka 2021, Pato la Taifa lilikua kwa wastani wa asilimia 4.9 ikilinganishwa na maoteo ya ukuaji wa asilimia 5.0 na ukuaji halisi wa asilimia 4.8 mwaka 2020. Kuimarika kwa kasi ya ukuaji wa uchumi kulitokana na kuongezeka kwa: uwekezaji hususan katika miundombinu ya afya, elimu, nishati, maji, ujenzi wa barabara, reli na viwanja vya ndege; shughuli za kiuchumi zilizotokana na ongezeko la mikopo katika sekta binafsi; na uzalishaji wa madini (dhahabu na makaa ya mawe). Shughuli za uchumi zilizokua kwa kasi kubwa kwa kipindi husika ni pamoja na: sanaa na burudani (asilimia 19.4); umeme (asilimia 10.0); madini (asilimia 9.6); na habari na mawasiliano (asilimia 9.1). Kiwango cha ukuaji wa uchumi wa Tanzania kinaonekana kuwa kidogo ikilinganishwa na baadhi ya nchi za SADC na EAC kutokana na nchi hizo kutokea kwenye ukuaji wa kiwango hasi kwa mwaka 2020 kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na. 1.2**. Ukuaji wa shughuli za kiuchumi katika mwaka 2021 ni kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 1.1**.


Kielelezo Na. 1.1: Ukuaji wa Shughuli za Kiuchumi Katika Pato la Taifa Mwaka 2021



9. Katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022, Pato la Taifa lilikua kwa asilimia 5.2 ikilinganishwa na asilimia 4.4 kwa kipindi kama hicho mwaka 2021. Ukuaji huo wa Pato la Taifa ulichangiwa na ukuaji wa shughuli mbalimbali za kiuchumi katika kipindi cha Januari hadi Juni, 2022. Sekta zilizokuwa na ukuaji mkubwa ni pamoja na: Maji safi na maji taka (asilimia 10.7); fedha na Bima (asilimia 10.0); habari na

mawasiliano (asilimia 8.6), umeme (asilimia 8.5), uchimbaji madini na mawe (asilimia 7.1). **Kielelezo Na 1.2** kinaonesha mwenendo wa ukuaji wa shughuli za uchumi kwa baadhi ya sekta kwa baadhi ya sekta katika nusu ya kwanza mwaka 2021 na 2022.

Kielelezo Na 1.2: Mwenendo wa ukuaji wa shughuli za uchumi kwa baadhi ya sekta, nusu ya kwanza mwaka 2021 na 2022.




1.4.2 Mwelekeo wa Pato la Taifa

10. Pato la Taifa mwaka 2022, linatarajiwa kukua kwa asilimia 4.7 ikilinganishwa na ukuaji halisi wa asilimia 4.9 mwaka 2021. Makadirio haya yanatokana na changamoto zinazoukabili uchumi wa dunia ikiwemo athari za janga la UVIKO - 19 na vita nchini Ukraine ambavyo vimesababisha ongezeko la bei za bidhaa mbalimbali nchini hususan petroli, ngano, mafuta ya kula na mbolea. Makadirio haya ni zaidi ya wastani wa ukuaji wa nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara wa asilimia 3.8 mwaka 2022. Hata hivyo, katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022, viashiria vingi vya uchumi vilikuwa na mwenendo wa kuridhisha ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa uzalishaji wa saruji (asilimia 18.7); umeme (asilimia 13.7); bidhaa zinazouzwa nje (asilimia 44.3). Aidha, idadi ya watalii waliotembelea Tanzania iliongezeka kutoka 637,052 mwaka 2020/21 hadi 1,123,130 mwaka 2021/22 ambapo mapato yaliongezeka kwa asilimia 183 katika kipindi husika. Vile vile, hatua zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali za kuwekeza kwenye miradi ya maendeleo zitachochea shughuli za kiuchumi, kuongeza ushiriki wa sekta binafsi katika kutekeleza miradi hiyo na pia kuongeza fursa za ajira na kipato.

11. Katika mwaka 2023, ukuaji wa Pato la Taifa unatarajiwa kuongezeka hadi asilimia 5.3 na kufikia wastani wa asilimia 6.3 katika muda wa kati (2023 - 2025). Ukuaji huo utaendana na jitihada zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali kuimarisha uchumi kutokana na athari za UVIKO - 19 na vita nchini Ukraine;

utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwemo miundombinu ya nishati, usafiri na usafirishaji na huduma za jamii ambayo ni muhimu katika kuchochea shughuli za kiuchumi na kuongeza fursa za ajira; kuimarishwa kwa ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya ndani na usimamizi wa matumizi; kuendeleza ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi; kuendelea kuboresha sekta ya utalii; na kuimarisha usimamizi na udhibiti wa uchimbaji wa madini. Ukuaji na mwelekeo wa uchumi wa Tanzania ni kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 1.3**.


Kielelezo Na. 1.3: Ukuaji na Mwelekeo wa Uchumi wa Tanzania



1.4.3 Mwenendo na Mwelekeo wa Mfumuko wa Bei

12. Katika mwaka 2021/22, mfumuko wa bei Tanzania ulifikia wastani wa asilimia 4.0 ambao ni ndani ya malengo ya kati ya asilimia 3.0 hadi 5.0 na vigezo vya mtangamano wa kiuchumi kikanda (EAC na SADC). Mfumuko wa bei katika kipindi cha marejeo uliongezeka kutokana na: kupanda kwa bei za bidhaa (mafuta ya kula, mbolea, na petroli) kufuatia kuvurugika kwa mnyororo wa uzalishaji na usambazaji wa bidhaa na huduma katika soko la dunia uliotokana athari za UVIKO - 19 na vita kati ya nchi za Urusi na Ukraine; na kupungua kwa upatikanaji wa mazao ya chakula kwa nchi jirani uliosababishwa na mabadiliko ya tabianchi hususan katika maeneo yanayotegemea mvua za vuli. Mwenendo wa Mfumuko wa Bei ni kama unavyoonekana katika **Kielelezo Na. 1.4**.

Kielelezo Na. 1.4: Mwenendo wa Mfumuko wa Bei (Juni 2018 – Juni 2022)



13. Mfumuko wa bei ulifikia asilimia 4.8 Septemba 2022 ikilinganishwa na asilimia 4.0 Septemba 2021. Katika muda wa kati, mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kubaki ndani ya lengo la nchi la kati ya asilimia 3.0 hadi 5.0 pamoja na kuendana na vigezo (*convergence criteria*) vilivyowekwa na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Matarajio ya kasi ndogo ya mfumuko wa bei yanatokana na: kupungua kwa gharama za uzalishaji kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa nishati ya gesi na umeme; na usimamizi madhubuti wa sera za fedha na bajeti. Aidha, uwekezaji katika miundombinu ya umwagiliaji na utoaji wa ruzuku ya mbolea unatarajiwa kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na hivyo kupunguza mfumuko wa bei.

1.4.4 Mwenendo wa Ujazi wa Fedha na Mikopo

14. Katika mwaka 2021/22, Benki Kuu iliendelea kutekeleza sera ya fedha inayolenga kuhakikisha uwepo wa ukwasi wa kutosha ili kusaidia kufufua shughuli za kiuchumi zilizoathiriwa na janga la UVIKO-19. Aidha, utekelezaji wa sera ya fedha unakusudia kufikia malengo mapana ya Serikali ya ukuaji wa uchumi na kudhibiti mfumuko wa bei ili uendelee kuwa ndani ya wigo wa asilimia 3.0 hadi 5.0. Kufuatia utekelezaji huo, mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa wastani wa asilimia 19.4 mwaka 2021/22, ikilinganishwa na lengo la ukuaji wa asilimia 10.6 na ukuaji halisi wa wastani wa asilimia 3.6 mwaka 2020/21. Ongezeko hili limechangiwa zaidi na utekelezaji wa sera ya fedha ya kuongeza ukwasi na kuimarika kwa mazingira ya kibiashara nchini. Aidha, kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi kulitokana na sera madhubuti za Serikali za kufungua uchumi na kuwezesha ushiriki wa sekta binafsi katika shughuli za biashara na uwekezaji. Hali hii pia ilisaidia wakopaji kuweza kurejesha mikopo yao na hivyo kuongeza utulivu wa sekta ya fedha

1.4.5 Mwenendo wa Viwango vya Riba

15. Katika mwaka ulioishia Juni 2022, viwango vya riba za mikopo kwa ujumla vilipungua kufikia wastani wa asilimia 16.41 kutoka asilimia 16.60 Juni 2021. Kupungua kwa riba za mikopo kulitokana na sera ya fedha iliyolenga kuongeza ukwasi na usimamizi wa hatua mbalimbali za kupunguza riba na mikopo chechefu, ikiwemo matumizi ya kanzidata ya taarifa ya kumbukumbu za wakopaji. Aidha, viwango vya riba za amana kwa ujumla viliongezeka kufikia wastani wa asilimia 6.80 mwaka 2021/22 kutoka wastani wa asilimia 6.75 mwaka 2020/21. Hii inatokana na kuongezeka kwa ushindani katika taasisi za fedha. Riba za mikopo ya mwaka mmoja zilifikia wastani wa asilimia 16.73 Juni 2022 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 16.58 katika kipindi kama hicho mwaka 2021. Kwa upande mwingine, riba za amana za mwaka mmoja zilifikia wastani wa asilimia 8.03 katika kipindi kilichoishia Juni 2022 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 8.43 Juni 2021.

1.4.6 Mwenendo wa Viwango vya Ubadilishaji Fedha

16. Thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya sarafu mbalimbali duniani imeendelea kuwa tulivu katika kipindi chote cha mwaka 2021/22. Hali hii imechangiwa kwa kiasi kikubwa na utulivu wa bei nchini; utekelezaji madhubuti wa sera za fedha na bajeti; na uwepo wa akiba ya kutosha ya fedha za kigeni. Katika kipindi hicho, dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,313.96 ikilinganishwa na shilingi 2,310.18 katika kipindi kama hicho mwaka 2020/21.

1.4.7 Mwenendo wa Sekta ya Benki

17. Katika mwaka 2021/22, mapato na faida kutokana na uwekezaji katika rasilimali na mtaji yaliongezeka ikilinganishwa na mwaka 2020/21. Katika kipindi hicho, faida ya benki itokanayo na mali (*Returns on Asset - ROA*) ilifikia wastani wa asilimia 4.1 kutoka wastani wa asilimia 2.4 mwaka 2020/21 na faida ya benki itokanayo na mtaji (*Returns on Equity - ROE*) ilifikia wastani wa asilimia 18.4 kutoka wastani wa asilimia 10.4 mwaka 2020/21. Katika kipindi hicho, uwiano wa mikopo chechefu ulipungua kufikia wastani wa asilimia 7.8 ya mikopo yote kutoka asilimia 9.3 kwa mwaka ulioishia Juni 2021. Mwenendo huu unaonesha kuendelea kuimarika kwa sekta ya benki ambapo kumekuwa na mtaji na ukwasi wa kutosha kukidhi mahitaji ya kila siku ya wenye amana na wakopaji na kuimarika kwa thamani ya rasilimali za benki nchini. Benki Kuu itaendelea kuhakikisha thamani ya rasilimali za benki nchini inaendelea kuimarika kwa kuchukua hatua madhubuti ili kupunguza mikopo chechefu kufikia lengo la kutozidi asilimia 5.0.

1.4.8 Mwenendo wa Sekta ya Nje

18. Sekta ya nje imeendelea kustahimili changamoto zitokanazo na vita kati ya nchi za Urusi na Ukraine na kuibuka kwa maambukizi mapya ya UVIKO-19 nchini China yaliyosababisha kufungwa kwa uzalishaji viwandani katika baadhi ya miji. Hali hii imesababisha kupanda kwa bei za bidhaa kutokana na kuathirika kwa

mfumo wa uzalishaji na usambazaji bidhaa duniani. Katika kipindi cha mwaka unaoishia Juni 2022, urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho wa mali nchi za nje ulifikia nakisi ya dola za Marekani milioni 3,766.9 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 1,789.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2021.

19. Katika kipindi cha mwaka unaoishia Juni 2022, thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje ilifikia dola za Marekani milioni 11,016.7 kutoka dola za Marekani milioni 8,811.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2021, sawa na ongezeko la asilimia 25.0. Hii, ilichangiwa na ongezeko la mapato yatokanayo na shughuli za utalii ambayo yaliongezeka kutoka dola za Marekani milioni 834.1 hadi dola za Marekani milioni 1,790.5. Aidha, kulikuwa na ongezeko katika mauzo ya bidhaa za viwandani kama vile chuma, bidhaa za chuma na nguo; bidhaa za maua na mbogamboga; pamoja na nafaka, hususan mchele na mahindi.

20. Thamani ya bidhaa na huduma ziliagizwa kutoka nje ziliongezeka kwa asilimia 39.4 na kufikia dola za Marekani milioni 13,715.7 katika kipindi cha mwaka unaoishia Juni 2022 kutoka dola za Marekani milioni 9,841.4 kwa kipindi kama hicho 2021. Hali hiyo ilitokana na kuongezeka kwa uagizaji wa malighafi, bidhaa za petroli, chuma na bidhaa za chuma pamoja na plastiki na malipo ya gharama za usafirishaji. Aidha, vita kati ya nchi za Urusi na Ukraine ilichangia ongezeko la thamani ya bidhaa zinazoagizwa nje kutokana na kuongezeka kwa bei za bidhaa hususan mafuta ya kula, ngano na mbolea.

21. Katika kipindi cha mwaka ulioishia Juni 2022, urari wa malipo ya kawaida uliongezeka kufikia nakisi ya dola za Marekani milioni 3,386.3 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 1,825.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2021. Hali hii ilichangiwa na kuongezeka kwa thamani ya bidhaa zilizoagizwa hususan mafuta ya petroli. Akiba ya fedha za kigeni nayo iliathiriwa na vita inayoendelea nchini Ukraine iliyosababisha kuongezeka kwa gharama za uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi. Akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani bilioni 5.11 Juni 2022, kiasi ambacho kinatosheleza uagizaji bidhaa na huduma nje ya nchi kwa kipindi cha miezi 4.6. Hata hivyo, kiwango hiki ni zaidi ya lengo la nchi la kukidhi miezi 4.0 na zaidi ya lengo la miezi 4.5 kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Jedwali Na. 1.4: Urari wa Malipo ya Kawaida

	2020/21	2021/22	Badiliko(%)
Urari wa Bidhaa	-2,100.10	-4,616.40	119.8
Mauzo nje	6,446.40	7,079.00	10.1
Uagizaji nje	8,546.60	11,713.40	37.1
Urari wa Huduma	1,069.70	1,917.40	79.2
Mapato	2,364.50	3,919.70	65.8
Malipo	1,294.90	2,002.40	54.6

Urari wa Bidhaa na huduma	-1,030.50	-2,699.00	161.9
Mauzo ya bidhaa na huduma	8,811.00	11,016.70	25
Uagizaji bidhaa na huduma	9,841.40	13,715.70	39.4
Urari wa Mapato ya vitega uchumi	-1,247.30	-1,277.00	2.4
Mapato	67.40	153.50	127.7
Malipo	1,314.70	1,430.50	8.8
Uhamisho wa mali	452.10	589.70	30.4
Zilizoingia	513.50	700.20	36.4
Kwa serikali kuu	76.70	122.40	59.7
Zilizotoka	61.40	110.50	80.2
Urari wa malipo ya kawaida	-1,825.60	-3,386.30	85.5

Chanzo: *Benki Kuu ya Tanzania*

1.5 Deni la Serikali

22. Deni la Serikali lilifikia shilingi bilioni 71,559.0 Juni 2022 kufuatia kupokelewa kwa mikopo mipya kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, viwanja vya ndege, umeme, elimu na afya. Aidha, deni la Serikali limeongezeka kutokana na kutolewa kwa hatifungani maalumu ya shilingi bilioni 2,176.7 kwa ajili ya kulipa deni la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) linalohusu michango ya watumishi waliokuwa kwenye utumishi kabla ya mwaka 1999. Aidha, tarehe 7 Oktoba 2022 kampuni ya Moody's Investors Service ambao ni wabobezi katika masuala ya kupima uhimilivu wa deni duniani walitoa taarifa inayoonesha kuwa mwelekeo wa hali ya uhimilivu wa deni la Tanzania umeimarika (positive outlook). Kampuni hiyo ilifanya uchambuzi wa athari ya uwezo wa nchi kukopa na kulipa madeni yake kwa kujitolea (unsolicited credit rating). Matokeo haya yanatokana na kuwepo kwa utulivu wa kisiasa nchini na hatua ya Serikali ya awamu ya sita katika kufungua uchumi.

23. Tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanyika Novemba 2021 ilionesha kuwa deni la Serikali limeendelea kuwa himilivu katika muda mfupi, wa kati na mrefu (**Jedwali Na.1.5**).

24. Serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuhakikisha kuwa deni linaendelea kuwa himilivu kwa:

- (i) Kuelekeza fedha za mikopo kwenye sekta za uzalishaji na miradi inayochochea kasi ya ukuaji wa uchumi na mauzo nje ya nchi;
- (ii) Kutoa kipaumbele kwenye mikopo yenye masharti nafuu (semi concessional loans);
- (iii) Kuimarisha mikakati ya kukusanya mapato ya ndani ili kuhakikisha sehemu kubwa ya bajeti inagharamiwa na mapato ya ndani;

- (iv) Kuweka mazingira rafiki ya kuvutia biashara na uwekezaji ili kuongeza fursa za kiuchumi (ajira, malighafi, kipato, mapato ya kodi); na
- (v) Kuimarisha usimamizi na udhibiti wa matumizi ya Serikali.

Jedwali Na. 1.5: Matokeo ya Tathmini ya Uhimilivu wa Deni kwa Mwaka 2021

Viashiria	Ukomo	20/21 ¹	21/22	22/23	23/24	24/25	25/26	26/ 27	31/ 32
Deni la Nje (Asilimia)									
Uwiano wa thamani halisi ya Deni kwa Pato la Taifa	40	18.8	18.8	18.7	18.8	18.8	18.5	18.4	20.2
Uwiano wa thamani halisi ya Deni kwa Mauzo ya Nje ya Nchi	180	142.4	132.9	117.4	108.5	102.8	96.9	93.7	95.7
Uwiano wa Ulipaji wa Deni kwa Mauzo ya Nchi	15	14.8	14.9	11.5	9.4	9.2	9.2	7.7	9.4
Uwiano wa Ulipaji wa Deni kwa Mapato	18	14.6	14.2	12.1	10.6	10.9	11.3	9.6	12.1
Deni la Ndani na Nje (Asilimia)									
Uwiano wa Thamani Halisi ya Deni kwa pato la Taifa	55	31	31.8	31.8	31.5	30.7	29.4	29	33
Uwiano wa Thamani Halisi ya Deni kwa Mapato	N/A	224.9	206.2	201.9	198.3	191.8	181.8	179.4	199.3
Uwiano wa Ulipaji wa Deni kwa Mapato	N/A	36.2	32.4	31.2	27.4	25.6	23	20.6	26.3

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango, 2021

¹ Uwiano halisi kwa kila kiashiria kwa mwaka 2020/21

SURA YA PILI
MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KWA
MWAKA 2021/22

2.1 Utangulizi

25. Sura hii inaelezea mapitio ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2021/22 kwa kuzingatia malengo na shabaha za bajeti. Mapitio haya yamebainisha mafanikio, changamoto na mikakati ya kuboresha uandaaji na utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2023/24.

2.2 Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2021/22

26. Utekelezaji wa mpango na bajeti ya Serikali kwa mwaka 2021/22, ulizingatia vipaumbele vilivyobainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26); Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025; Dira ya Maendeleo ya Afrika Mashariki 2050; Agenda 2063 ya Umoja wa Afrika; na Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030. Aidha, usimamizi katika utekelezaji ulizingatia sheria na miongozo mbalimbali ikiwa ni pamoja na: Sheria ya Bajeti, SURA 439; Sheria ya Fedha za Umma, SURA 348; na Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, SURA 134; na Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo Tanzania. Vile vile, Serikali ilisimamia utekelezaji wa Sera za Mapato na Matumizi za Muda wa Kati zilizolenga kuwezesha utekelezaji wa programu na miradi mbalimbali.

27. Bajeti ya Serikali iliyoidhinishwa kwa mwaka 2021/22 ilikuwa shilingi bilioni 36,681.9. Hata hivyo, Septemba 2021, Serikali ilifanya majadiliano na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na kufanikiwa kupata mkopo nafuu usiokuwa na riba kupitia dirisha la *Rapid Credit Facility* (RCF) wenye thamani ya shilingi bilioni 1,310.6 kwa ajili ya kukabiliana na athari za UVIKO-19 katika sekta za kiuchumi na kijamii. Kupatikana kwa mkopo huu pamoja na mapitio ya mwenendo wa utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa kipindi cha nusu mwaka ulisababisha bajeti ya Serikali kubadilika na kuwa shilingi bilioni 37,992.5 kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 2.1**.

Jedwali Na.2.1: Bajeti ya Serikali iliyoidhinishwa mwaka 2021/22

Shilingi Bilioni

	BAJETI ILYOIDHINISHWA 2021/22	BAJETI ILYOIDHINISHWA 2021/22 (SUPPLEMENTARY)
Mapato ya Ndani	26,384.7	25,691.7
Mapato ya Kodi	20,738.3	20,295.2
Mapato Yasiyo ya Kodi	5,646.5	5,396.5
Misaada	1,138.1	1,138.1
Mikopo ya Nafuu	1,817.8	3,128.5
Mikopo ya Kibiashara Nje	2,352.1	3,045.1
Mikopo ya Ndani	1,838.8	1,838.8
Kulipa Mtaji Deni la Ndani (Rollover)	3,150.3	3,150.3
JUMLA YA MAPATO	36,681.9	37,992.5
JUMLA YA MATUMIZI	36,681.9	37,992.5
Matumizi ya Kawaida	23,003.0	23,003.0
Mishahara	8,150.5	8,150.5
Malipo ya Riba	2,676.7	2,676.7
Mtaji Nje	3,051.4	3,051.4
Mtaji Ndani	3,150.3	3,150.3
Matumizi Mengineyo	5,974.0	5,974.0
Matumizi ya Maendeleo	13,678.9	14,989.5
Fedha za Ndani	10,723.0	10,723.0
Fedha za Nje	2,955.9	4,266.5

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

2.2.1 Mapato na Matumizi

28. Katika mwaka 2021/22, Serikali ilikadiria kukusanya na kutumia shilingi bilioni 37,992.5. Hadi Juni 2022, Serikali ilikusanya jumla ya shilingi bilioni 36,924.8 sawa na asilimia 97 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kiasi hiki kinajumuisha shilingi bilioni 24,395.6 mapato ya ndani sawa na asilimia 95 ya lengo la mwaka la shilingi bilioni 25,691.7; shilingi bilioni 4,825.3 ni misaada na mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo sawa na asilimia 113 ya lengo la shilingi bilioni 4,254.6; na shilingi bilioni 7,703.9 ni mikopo ya kibiashara ya ndani na nje ya nchi sawa na asilimia 96 ya lengo la mwaka la shilingi bilioni 8,034.2. Aidha, Serikali imetumia shilingi bilioni 37,215.8 kugharamia utekelezaji wa shughuli na miradi mbalimbali ya Serikali. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 22,561.8 ni matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 14,654.3 ni matumizi ya maendeleo. **Jedwali Na.2.2** linaonesha mchanganuo wa

makadirio ya mapato na matumizi pamoja na ufanisi katika eneo la mapato na matumizi.

Jedwali Na. 2.2: Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2021/22

Shilingi bilioni

	Bajeti	Halisi	Asilimia
Mapato ya Ndani	25,691.7	24,395.6	95
Mapato ya Kodi (TRA)	20,283.4	20,029.3	99
Mapato Yasiyo ya Kodi (TRA)	1,494.7	902.0	60
Mapato Yasiyo ya Kodi	3,049.8	2,574.8	84
Mapato ya Halmashauri	863.9	889.5	103
Misaada	1,138.1	708.5	62
Misaada ya Kibajeti	-	103.2	
Misaada ya Maendeleo	915.5	519.3	57
Mifuko ya Kisekta	222.6	86.0	39
Mikopo Nafuu	3,128.5	4,116.8	132
Mikopo Nafuu ya Kibajeti	1,310.7	1,291.7	99
Mikopo Nafuu ya Miradi ya Maendeleo	1,770.0	2,818.3	159
Mikopo Nafuu ya Mifuko ya Kisekta	47.8	6.8	14
Mikopo ya Kibiashara Kutoka Nje	3,045.1	1,809.5	59
Mikopo ya Kibiashara Kutoka Ndani	4,989.1	5,894.4	118
Mikopo ya Kugharamia Miradi	1,838.8	2,850.0	155
Mikopo ya Kulipa Mtaji Deni la Ndani	3,150.3	3,044.4	97
JUMLA YA MAPATO	37,992.5	36,924.8	97
Matumizi ya Kawaida	22,732.8	22,561.5	99
Mishahara	8,136.5	8,087.4	99
Mfuko Mkuu wa Serikali (Deni)	8,756.8	8,756.8	100
Matumizi Mengineyo & CFS	5,839.5	5,717.3	98
Matumizi ya Maendeleo	15,259.7	14,654.3	96
Miradi ya Fedha za Ndani	11,591.1	11,554.6	100
Miradi ya Fedha za Nje	3,668.6	3,099.7	84
JUMLA MATUMIZI	37,992.5	37,215.8	98

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

29. Ukusanyaji wa mapato ya ndani ulikua kwa asilimia 18.5 na kufikia shilingi bilioni 24,395.6 mwaka 2021/22 ikilinganishwa na makusanyo ya shilingi bilioni 20,594.7 mwaka 2020/21. Ongezeko hili la mapato ya ndani limetokana na: kuendelea kuimarika kwa mifumo ya kielektroniki katika usimamizi wa ukusanyaji wa mapato; kuboresha mazingira ya ufanyaji wa biashara na uwekezaji nchini; kuongezeka kwa ulipaji kodi wa hiari kutokana na mahusiano bora na walipakodi; kuongezeka kwa kiwango cha uhamasishaji na utoaji wa elimu kwa mlipakodi kupitia *Kampeni ya Mlango kwa Mlango*.

2.3 Mafanikio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti

30. Utekelezaji wa mpango na bajeti ya Serikali kwa mwaka 2021/22 umekuwa na mafanikio makubwa katika nyanja na sekta mbalimbali. Mafanikio hayo ni pamoja na:

31. **Ulipaji wa Mishahara:** Hadi Juni 2022, jumla ya shilingi bilioni 8,087.4 zimetumika kulipa mishahara kwa watumishi wa Umma sawa na asilimia 99.2 ya lengo la shilingi bilioni 8,150.5.

32. **Upandishaji Vyeo Watumishi:** Hadi Juni 2022, shilingi bilioni 160.0 zimetumika kwa ajili ya kugharamia upandishaji vyeo watumishi 126,814 waliostahili.

33. **Ulipaji wa Madai ya Malimbikizo ya Mishahara kwa Watumishi wa Umma:** Kwa kipindi cha kuanzia Julai 2021 hadi Juni 2022 madai ya malimbikizo ya mishahara yenye jumla ya shilingi bilioni 131.1 yamelipwa kwa watumishi 76,866, ambapo kati ya kiasi hicho shilingi bilioni 124.3 zimelipwa kwa watumishi 74,798 ambao utumishi wao haujakoma na shilingi bilioni 6.8 kwa watumishi 2,068 waliostaafu.

34. **Ulipaji wa Madeni ya Utekelezaji wa mashauri ya kimkataba, Makandarasi, Wazabuni, Watumishi na Watoa Huduma:** Hadi Juni 2022, Serikali imehakiki na kulipa madeni yenye jumla ya shilingi bilioni 796.7. Kati ya kiasi hicho, mashauri ya kimkataba shilingi bilioni 588.3, wakandarasi shilingi bilioni 4.2, wazabuni shilingi bilioni 92.6, watumishi (yasiyo ya kimshahara) shilingi bilioni 24.5 na watoa huduma na madeni mengineyo shilingi bilioni 87.1.

35. **Ulipaji wa Deni la Serikali:** Hadi Juni 2022, Serikali ilitumia shilingi bilioni 8,756.8 sawa na asilimia 100 ya lengo kwa ajili ya kulipa mitaji na riba ya mikopo mbalimbali. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 5,869.8 zilitumika kulipa mitaji sawa na asilimia 100 ya lengo na shilingi bilioni 2,887.0 zilitumika kulipa riba sawa na asilimia 100 ya lengo.

2.3.1 Mafanikio katika Utekelezaji wa Miradi ya Kielelezo na Kimkakati

36. Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuendelea kwa Ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa (SGR), Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere - JNHPP (MW 2,115), Usambazaji wa Umeme Vijijini; Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia - (Liquefied Natural Gas - LNG) na Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania), (*East African Crude Oil Pipeline - EACOP*). Maelezo ya kina kuhusu mafanikio katika Utekelezaji wa Miradi ya Kielelezo na Kimkakati yanapatikana katika Mapendekezo ya Mpango wa Mwaka 2023/24.

2.3.2 Changamoto zilizojitokeza Katika Utekelezaji wa Bajeti

37. Licha ya mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2021/22 changamoto zilizojitokeza ni pamoja na:

- (i) Vita nchini Ukraine ambayo imedhoofisha matarajio ya kurejea kwa shughuli za kiuchumi zilizokuwa zimeathiriwa na UVIKO-19. Hivyo, kasi ya ukuaji wa

uchumi inatarajiwa kupungua kufikia asilimia 4.7 mwaka 2022 ikilinganishwa na matarajio ya awali ya asilimia 5.2;

- (ii) Kuongezeka kwa bei na gharama za usafirishaji wa bidhaa na huduma kutoka nje, hususan bidhaa za petroli, mafuta ya kula, mbolea kutokana na athari za vita nchini Ukraine;
- (iii) Kukosekana kwa mazingira wezeshi ya matumizi ya teknolojia kwa baadhi ya Wizara, Taasisi za Umma na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Mfano ulipaji wa kodi ya ardhi, leseni za biashara; na
- (iv) Kuendelea kuwepo kwa baadhi ya wafanyabiashara wanaokwepa kodi hususan kupitia njia za magendo, uhamishaji wa faida kwa kampuni zenye mtandao wa kimataifa na kutokutoa stakabadhi za kielektroniki wakati mauzo yanapofanyika hivyo kuathiri ukusanyaji wa mapato yatokanayo na kodi.

2.3.3 Hatua Zilizochukuliwa Kukabiliana na Changamoto

38. Katika kukabiliana na changamoto hizo, Serikali imeendelea kuchukua hatua zifuatazo:

- (i) Kuendelea kuongeza tija katika sekta za uzalishaji ili kupunguza utegemezi wa uagizaji bidhaa kutoka nje ikiwemo sekta za kilimo, mifugo, uvuvi, nishati;
- (ii) Kuendelea kutoa ruzuku katika bidhaa za petroli na pembejeo za kilimo kwa lengo la kupunguza gharama za maisha kwa wananchi;
- (iii) Kuendelea kusimamia kikamilifu utekelezaji wa bajeti na mipango yenye lengo la kuongeza uzalishaji na mauzo nje;
- (iv) Kuendelea kufuatilia kwa karibu mwenendo wa biashara duniani ili kuchangamkia fursa zitokanazo na athari za UVIKO-19 na vita kati ya Urusi na Ukraine, hususan uzalishaji wa mazao ya biashara na chakula pamoja na kuchukua hatua za kisera na kiutawala kurejesha biashara zilizoathirika;
- (v) Kuendelea kutekeleza miradi ya kimkakati ya kuongeza mapato ya ndani na kutafuta masoko ya bidhaa nje ili kuongeza uwezo wa Serikali kugharamia mpango na bajeti;
- (vi) Kuendelea kuimarisha mifumo ya usimamizi na ukusanyaji wa mapato ili kudhibiti ukwepaji kodi pamoja na kuhamasisha umma juu ya umuhimu wa kulipa kodi, matumizi ya stakabadhi za kielektroniki na kuhimiza malipo ya Serikali kwa kutumia namba ya kumbukumbu ya malipo; na
- (vii) Kuimarisha usimamizi wa mapato yasiyo ya kodi katika Wizara na Idara Zinazojitegemea ili kuhakikisha mikakati iliyopangwa ya kuongeza mapato inatekelezwa ipasavyo ili kuongeza ufanisi.

SURA YA TATU
MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MWONGOZO WA MAANDALIZI YA
MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2022/23

3.1 Utangulizi

39. Sura hii inaeleza mapitio ya utekelezaji wa Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2022/23. Mapitio hayo yamefanyika kwa kuzingatia utekelezaji wa maelekezo yaliyotolewa katika mwongozo huo, mrejesho wa vikao vya uchambuzi wa bajeti za Mafungu kwa mwaka 2022/23, maoni ya wadau katika vikao vya mapitio ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2021/22, maandalizi ya bajeti ya mwaka 2022/23 pamoja na maoni ya wadau yaliyotolewa katika vikao kazi mbalimbali vya Serikali kuhusu maandalizi na utekelezaji wa bajeti ya Serikali.

3.2 Muundo wa Bajeti ya Mwaka 2022/23

40. Mwongozo wa Maandalizi ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/23, ulipendekeza kukusanya na kutumia jumla ya shilingi bilioni 39,387.5. Kufuatia vipaumbele vya Serikali na maboresho mbalimbali ya kisera yaliyofanyika wakati wa uidhinishaji wa bajeti, Mfumo wa bajeti ya Serikali ulibadilika kutoka mapendekezo ya shilingi bilioni 39,387.5 hadi shilingi bilioni 41,480.6 sawa na ongezeko la shilingi bilioni 2,093.1 kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 3.1**.

Jedwali Na. 3.1: Mapendekezo ya Bajeti ya Mwongozo na Bajeti ya Serikali Iliyoidhinishwa kwa mwaka 2022/23

Shilingi Bilioni

Jedwali Na.1 : Mapendekezo ya Bajeti ya Mwongozo na Bajeti iliyoidhinishwa			
Shilingi Bilioni			
		Mapendekezo ya Bajeti ya Mwongozo	Bajeti Iliyoidhinishwa
A	Mapato ya Ndani	28,568	28,018
	Mapato TRA (Kodi na yasiyo ya Kodi)	24,238	23,653
	Mapato Yasiyo ya Kodi (Wizara, Idara na Msajili wa Haziri)	3,393	3,353
	Mapato ya Halmashauri	937	1,012
B	Misaada	1,117	1,101
	Misaada ya Kibajeti	-	56
	Misaada ya Miradi ya Maendeleo	824	924
	Misaada ya Mifuko ya Kisekta	293	122
C	Mikopo Nafuu	1,926	3,547
	Mikopo Nafuu ya Kibajeti	-	1,894
	Mikopo Nafuu ya Miradi ya Maendeleo	1,869	1,653
	Mikopo Nafuu ya Mifuko ya Kisekta	58	-
D	Mikopo ya Ndani na Nje ya Masharti ya Kibiashara	7,776	8,814
	Mikopo ya Nje	2,422	3,034
	Mikopo ya Ndani	2,054	2,480
	Mikopo ya Ndani Kulipia Mtaji wa Deni la Ndani	3,300	3,300
	JUMLA YA MAPATO YOTE (A+B+C+D)	39,388	41,481
E	Matumizi ya Kawaida	25,847.8	26,474.6
	Mfuko Mkuu wa Serikali	11,592	11,308
	Mishahara	10,108	9,831
	Matumizi Mengineyo	4,148	5,335
F	Matumizi ya Maendeleo	13,539.7	15,006.0
	Fedha za Ndani	10,496	12,307
	Fedha za Nje	3,043	2,699
	JUMLA MATUMIZI YOTE (E+F)	39,388	41,481

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

3.3 Mwenendo wa Utekelezaji wa Bajeti kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2022/23

3.3.1 Mapato

41. Mapato yaliyokusanywa kutoka vyanzo vyote vya ndani na nje kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2022/23 ni shilingi bilioni 9,181.8. Kati ya mapato hayo, mapato ya ndani yalifikia shilingi bilioni 6,293.1 sawa na asilimia 96.3 ya lengo la shilingi bilioni 6,537.0. Mapato ya ndani yanajumuisha; shilingi bilioni 5,582.7 zilizokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania; shilingi bilioni 470.2 ni mapato yasiyo ya kodi yanayokusanywa na Wizara, Idara Zinazojitegemea na Taasisi; na

shilingi bilioni 240.2 ni mapato kutoka vyanzo vya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, misaada na mikopo nafuu ilifikia shilingi bilioni 956.0 sawa na asilimia 98.4 ya lengo la shilingi bilioni 971.1. Vile vile, mikopo ya kibiashara kutoka masoko ya ndani ilifikia shilingi bilioni 1,689.6 sawa na asilimia 85.5 ya lengo la shilingi bilioni 1,975.1. Mikopo ya kibiashara kutoka nje ilifikia shilingi bilioni 243.1 sawa na asilimia 66.5 ya lengo la shilingi bilioni 365.6. Serikali inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ili kuhakikisha malengo ya mapato yaliyowekwa kwa mwaka 2022/23 yanafikiwa.

3.3.2 Matumizi

42. Katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2022/23 ridhaa ya matumizi ya shilingi bilioni 9,153.8 ilitolewa sawa na asilimia 92.9 ya lengo la shilingi bilioni 9,848.9. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 5,848.7 ni ridhaa ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 3,305.1 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo sawa na asilimia 36.1 ya matumizi yote kwa kipindi cha robo mwaka. Fedha za matumizi ya kawaida zilizotolewa zinajumuisha: shilingi bilioni 2,233.5 kwa ajili ya mishahara; shilingi bilioni 1,513.8 kwa ajili ya kugharamia deni la Serikali na matumizi mengine ya Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali; na shilingi bilioni 2,101.4 kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, fedha za maendeleo zilizotolewa zinajumuisha shilingi bilioni 2,698.9 fedha za ndani na shilingi bilioni 606.2 fedha za nje. Kiasi cha shilingi bilioni 588.7 ni fedha za Washirika wa Maendeleo zilizopelekwa moja kwa moja kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

43. Katika mwaka 2022/23, Serikali imedhamiria kufanya mapitio ya utekelezaji wa bajeti kwa kila robo mwaka. Mapitio haya yataiwezesha Serikali kubaini mwenendo wa utekelezaji wa bajeti ili kupata matokeo yanayotarajiwa.

3.4 Utekelezaji wa Maelekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2022/23

Mapitio ya utekelezaji wa maelekezo yaliyotolewa katika Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2022/23 ni kama ifuatavyo:

44. **Uzingatiaji wa Ratiba ya Maandalizi ya Mpango na Bajeti:** Kwa kuzingatia cha Sheria ya Bajeti, SURA 439, Kifungu Na. 15 (1) Kamati ya Kitaifa ya maandalizi ya Mwongozo iliundwa na kukamilisha jukumu lake kwa wakati. Mwongozo huo uliidhinishwa na Mamlaka zote zinazohusika ndani ya Serikali na Bunge kwa muda uliopangwa na kusambazwa kwa wadau mbalimbali mwezi Novemba, 2021.

45. Mapitio ya utekelezaji yameonesha kuwa, ratiba ya maandalizi ya Mpango na Bajeti ilizingatiwa na Maafisa Masuuli kama ilivyoelekezwa kwenye Mwongozo ambapo vitabu vya mapendekezo ya Mpango na Bajeti viliwasilishwa Wizara ya

Fedha na Mipango kwa ajili ya uchambuzi na hatua nyingine muhimu. Aidha, mapendekezo ya mipango na bajeti yaliwasilishwa katika Kamati husika za Kudumu za Bunge kwa wakati mwezi Machi, 2022.

46. **Uzingatiaji wa Masuala ya Muungano:** Katika uandaaji wa mpango na bajeti ya mwaka 2022/23 masuala ya Muungano yalizingatiwa kwa kutengewa bajeti kwa ajili ya uendeshaji wa vikao vya ushirikiano kati ya Wizara/Taasisi za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na miradi inayotekelezwa pande mbili za Muungano. Baadhi ya miradi/programu za maendeleo zinazotekelezwa kwa upande wa Zanzibar ni pamoja na: Mpango wa Kususuru Kaya Masikini kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) ambao umetengewa shilingi bilioni 17.76; Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge (MKURABITA) shilingi milioni 491 na Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo shilingi bilioni 1.4.

47. **Matumizi ya Fedha za Mapato ya Ndani kulingana na Makundi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa:** Jumla ya Halmashauri 22 zenye uwezo wa kukusanya mapato ya ndani zaidi ya shilingi bilioni 5 zilizowekwa katika Daraja A na Halmashauri 162 zilizokusanya mapato chini ya shilingi bilioni 5 ziliwekwa katika Daraja B. Halmashauri za Daraja A zilitenga asilimia 60 ya bajeti ya mapato yasiyolindwa sawa na shilingi bilioni 229.2 kwa ajili ya maendeleo na asilimia 40 ya bajeti ya mapato yasiyolindwa sawa na shilingi bilioni 124.0 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Halmashauri za daraja B zilitenga asilimia 40 ya bajeti ya mapato yasiyolindwa sawa na shilingi bilioni 165.6 kwa ajili ya maendeleo na asilimia 60 sawa na shilingi bilioni 234.5 kwa ajili ya matumizi ya kawaida kama ilivyoelekezwa.

48. Halmashauri za daraja A zilitenga shilingi bilioni 22.9 ikiwa ni asilimia 10 ya mapato ya ndani ya bajeti yasiyolindwa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya barabara zinazosimamiwa na Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (Tanzania Rural and Urban Roads Agency - TARURA). Aidha, baadhi ya miradi iliyotumia fedha za mapato ya ndani iliyotolewa na halmashauri ilihusu ujenzi wa miundombinu ya vituo vya afya, zahanati na vyumba vya madarasa yaliyochangiwa na nguvu za wananchi.

49. **Utengaji wa Asilimia 10 ya Bajeti ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri kwa ajili ya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu:** Halmashauri zote zilizingatia maelekezo ya mwongozo ya kutenga asilimia 10 ya mapato ya ndani yasiyolindwa kwa ajili ya mikopo ya Wanawake (asilimia 4), Vijana (asilimia 4) na Watu Wenye Ulemavu (asilimia 2). Taarifa ya mikopo ya asilimia 10 iliyotengwa kwa kila Halmashauri kwa mwaka 2022/23 na iliyotolewa kwa mwaka 2021/22 imeainishwa katika **Kiambatisho A1 na A2**. Aidha, halmashauri zimeanza kutumia mfumo wa

utoaji mikopo ya asilimia 10 (Ten Percent Loan Management Information System - TPLMIS) ili kuboresha utoaji wa mikopo hiyo. Vile vile, halmashauri zimeendelea kusesitizwa kuweka nguvu za ziada katika ufuatiliaji wa marejesho ya mikopo hiyo kwa mujibu wa marekebisho ya kanuni za utoaji na usimamizi wa mikopo ya mwaka 2021 ili kunufaisha vikundi vingi zaidi kutokana na utoaji wa mikopo.

50. **Utendaji wa Kamati za Bajeti:** Kamati za Bajeti ziliundwa kwa mujibu wa Sheria ya Bajeti, SURA ya 439 Kifungu cha 18(2) na Kanuni ya 17(2). Hata hivyo, katika vikao vya mapitio ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2021/22 na maandalizi ya bajeti ya mwaka 2022/23 ilibainika uwepo wa mapungufu ambayo ni: baadhi ya taasisi kutounda kamati za bajeti; kutoitisha vikao na kutozingatia muundo sahihi wa wajumbe wanaopaswa kuunda kamati hizo kisheria. Hivyo, bado upo umuhimu wa kuziimarisha Kamati hizo kwa kuzijengea uwezo na kutoa ufafanuzi sahihi wa kikanuni ili kuhakikisha zinatekeleza majukumu yake kikamilifu.

51. **Maandalizi ya Bajeti ya Mishahara:** Maandalizi ya bajeti ya mishahara yamekuwa yakizingatia miongozo na nyaraka mbalimbali zinazotolewa na Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (OR - MUUB) na Wizara ya Fedha na Mipango. Pamoja na maandalizi hayo, kumekuwa na changamoto ya mahitaji makubwa ya masuala ya mishahara ikilinganishwa na bajeti halisi inayoidhinishwa.

52. **Utengaji wa Bajeti na Usimamizi wa Miradi ya Maendeleo:** Miradi ya maendeleo ikijumuisha na usimamizi wake imeendelea kutengewa fedha kama ilivyoelekezwa. Hata hivyo, baadhi ya wizara za kisekta zimeendelea kutenga bajeti katika mafungu yao kwa shughuli ambazo zinatekelezwa katika ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hali hii husababisha changamoto ya utekelezaji na usimamizi wa miradi ya maendeleo. Aidha, katika usimamizi wa miradi kumekuwepo na changamoto ya uratibu ndani ya Mafungu kwa bajeti ya ufuatiliaji na tathmini kutotengwa katika vitengo stahiki, upungufu wa wataalam na baadhi ya miradi kusimamiwa na idara zisizohusika.

53. **Uingizaji wa Takwimu za Bajeti ya Serikali kwenye Mifumo ya CBMS na PlanRep:** Uchambuzi wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2022/23 umebaini kuwa Wizara, Sekretariati za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma na Wakala za Serikali zilikamilisha uingizaji wa takwimu sahihi za bajeti kwenye Mifumo ya CBMS na PlanRep kwa kuzingatia muda uliopangwa. Hata hivyo, kuna uhitaji wa kuendelea kutoa mafunzo ya matumizi ya mifumo hiyo kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo: mabadiliko ya watumishi na teknolojia ya mifumo.

54. **Matumizi ya Mfumo wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato - GePG:** Maafisa masuuli wameendelea kutumia mfumo wa GePG katika malipo ya huduma za Serikali kupitia Kumbukumbu namba ya Malipo (*control number*). Aidha, mfumo umeendelea kuboreshwa ili kukidhi mahitaji ya watumiaji na kuendana na mabadiliko ya teknolojia. Hadi mwezi Julai 2022, taasisi zilizounganishwa na zinazokusanya mapato kupitia mfumo huu zilifikia taasisi 543.

55. **Hatua za Kudhibiti Matumizi:** Mapitio ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2021/22 na maandalizi ya bajeti ya mwaka 2022/23 yamebainisha kuwa baadhi ya maelekezo hayakuzingatiwa kikamilifu ikiwemo kuendelea kuzalisha madeni. Pamoja na hatua nyingine, Maafisa Masuuli wameendelea kusisitizwa kuzingatia miongozo husika ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa bajeti ya Serikali. Miongozo hiyo ni pamoja na: Mwongozo wa Utaratibu wa Maombi na Utoaji wa Fedha katika utekelezaji wa Bajeti ya Serikali; Waraka wa Hazina Na. 1 wa Mwaka 2022 kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ya mwaka 2022/23; na Waraka wa Utumishi wa Umma Na.1 wa mwaka 2021 kuhusu matumizi ya mfumo mpya wa usimamizi wa taarifa za rasilimali watu na mishahara (New Human Capital Management Information System - HCMIS).

56. **Uwasilishaji wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti:** Maafisa Masuuli wanapaswa kuwasilisha taarifa za utekelezaji kila robo mwaka inapokamilika kwa mujibu wa Kifungu Na. 55(4) na Kanuni ya 29(5) za Sheria ya Bajeti, SURA 439. Aidha, imebainika kuwa ipo changamoto ya uwasilishaji wa taarifa kwa usahihi na wakati. Hivyo, upo umuhimu wa kuendelea kuhimiza, kufanya vikao vya pamoja vya uratibu na kufuatilia uwasilishaji wa taarifa mbalimbali za utekelezaji kwa wakati ikiwemo kuzingatia matumizi ya Dashibodi ya Ofisi ya Waziri Mkuu ili kuhakikisha taarifa za ufuatiliaji na tathmini kwa miradi ya maendeleo zinaandaliwa kwa usahihi na wakati.

57. **Uzingatiaji Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada:** Serikali imeendelea kupokea misaada na mikopo nafuu katika programu na miradi mbalimbali ya maendeleo kwa kuzingatia Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura 134. Hata hivyo, kumekuwa na changamoto katika upokeaji na matumizi ya fedha za misaada zilizo nje ya bajeti iliyoidhinishwa zinazotolewa na Asasi zisizo za Serikali katika Wizara, Taasisi, Mashirika ya Umma na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

58. **Utekelezaji wa Masuala Mtambuka:** Mafungu yameendelea kutenga bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa masuala mtambuka ikiwemo: Mikakati ya Mapambano dhidi ya rushwa; jinsia; utunzaji wa mazingira; mabadiliko ya tabianchi; utawala bora; dawa za kulevyu; UKIMWI na magonjwa yasiyo ambukiza; lishe pamoja na watu wenye ulemavu na wazee. Hata hivyo, utengaji wa bajeti katika masuala mtambuka umekuwa kikwazo kwa baadhi ya mafungu kutokana na ufinyu wa bajeti.

59. Uzingatiaji wa Maelekezo kwa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa:

(a) Uzingatiaji wa Maelekezo ya Jumla: Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ziliendelea kuzingatia maelekezo ya jumla ya Mwongozo wa Mpango na Bajeti wa Mwaka 2022/23. Aidha, zipo changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa maelekezo hayo ikiwa ni pamoja na: baadhi ya Halmashauri kutotumia kikamilifu mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji wa mapato; kutotengwa fedha za ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa; kutotengwa fedha kwa ajili ya kuwajengea uwezo wataalamu; kutotengwa fedha kwa ajili ya ununuzi wa viudadu ili kutokomeza mazalia ya mbu; na kutotengwa fedha kwa ajili ya kutatua migogoro, kulipa fidia, kutambua maeneo ya mipaka na kuweka alama za mipaka katika Halmashauri, Kata, Vijiji/Mitaa na Vitongoji pamoja na maeneo ya hifadhi.

(b) Uzingatiaji wa Maelekezo kuhusu Sekta za Afya, Elimu na Kilimo: Mamlaka za Serikali za Mitaa zimetenga jumla ya shilingi bilioni 15.0 kwa ajili ya kutekeleza afua za lishe kwa jamii ambapo tathmini inaonesha kuwa jamii imeendelea kuzingatia lishe bora na hivyo kuimarisha nguvu kazi. Pamoja na juhudi hizo, kutokuwa na bajeti ya kutosha na idadi ndogo ya watumishi kumesababisha changamoto katika utambuzi, usajili na utengamanisho kwa watoto walio katika mazingira hatarishi. Vile vile, kumekuwa na changamoto ya upatikanaji wa vifaa, vifaa-tiba na dawa katika baadhi ya hospitali za wilaya, vituo vya afya na zahanati suala linalochangia utoaji wa huduma hafifu za afya kwa jamii.

Kwa upande wa elimumsingi, bajeti imeendelea kutengwa kwa ajili ya uandikishwaji wanafunzi na usajili wa shule mpya. Hata hivyo, kumekuwepo na changamoto ya kutofautiana kwa muda wa upangaji wa bajeti ya Serikali na muda kikomo wa uandikishaji wanafunzi wa elimu ya awali na usajili wa shule mpya, hivyo kutokuwa na takwimu sahihi za kibajeti.

Katika Sekta ya Kilimo, Halmashauri zimekuwa zikitenga bajeti kutokana na makusanyo ya mapato ya ndani kwa ajili ya kuendeleza shughuli za kilimo (asilimia 20), mifugo (asilimia 15) na uvuvi (asilimia 5). Hata hivyo, utoaji wa fedha katika shughuli za sekta hiyo umekuwa siyo wa kuridhisha kama ilivyoelekezwa katika miongozo husika.

SURA YA NNE

MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2023/24

4.1 Utangulizi

60. Sura hii inaainisha malengo na shabaha ya uchumi jumla, misingi ya uchumi jumla, sera za bajeti na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2023/24 na katika muda wa kati. Sera za bajeti zinajumuisha sera za mapato, sera za matumizi pamoja na sera za misaada na mikopo. Sera hizi zimejikita katika kutekeleza dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26, wenye dhima ya *“Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu”*. Makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2023/24 na muda wa kati yamezingatia hali ya uchumi wa Tanzania na dunia.

4.2 Malengo na Shabaha ya Uchumi Jumla

61. Mwaka 2022, Pato Halisi la Taifa linakadiriwa kukua kwa asilimia 4.7 na kuongezeka hadi asilimia 5.3 mwaka 2023; mfumuko wa bei unatarajiwa kubaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia 3.0 – 5.0 katika kipindi cha muda wa kati; mapato ya kodi kufikia asilimia 12.0 ya Pato la Taifa kwa mwaka 2023/24 kutoka asilimia 11.7 ya mwaka 2022/23; mapato ya ndani kufikia asilimia 14.8 ya Pato la Taifa mwaka 2023/24 kutoka matarajio ya asilimia 14.9 mwaka 2022/23; nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) kuwa chini ya asilimia 3.0 ya Pato la Taifa; kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4); na kuhakikisha kuwa viashiria vya ustawi wa jamii vinaimarika.

4.3 Misingi ya Uchumi Jumla

62. Misingi itakayozingatiwa kufikia shabaha ya uchumi jumla ni pamoja na: kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi kwenye shughuli za uwekezaji na biashara; kuendelea kuhimili athari za majanga ya asili na yasiyo ya asili; kuendelea kuhimili athari zitokanazo na kushuka kwa uchumi wa dunia na kuongezeka kwa bei za bidhaa na huduma katika soko la dunia; kuendelea kuimarika kwa utoshelevu wa chakula nchini; na uwepo wa amani, usalama, umoja na utulivu wa ndani na nchi jirani.

4.4 Vipaumbele katika mwaka 2023/24

63. Katika mwaka 2023/24, maeneo yatakayopewa kipaumbele ni pamoja na kugharamia: miradi ya kielelezo inayoendelea; deni la Serikali; mishahara ya watumishi wa Umma; na huduma za jamii zikiwemo afya, elimu na maji. Aidha, Serikali itaweka msukumo katika kuimarisha sekta za uzalishaji na kuongeza kasi ya kufufua uchumi ulioathiriwa na UVIKO – 19, vita inayoendelea nchini Ukraine na mabadiliko ya tabianchi.

4.5 Mfumo wa Makadirio ya Mapato na Matumizi wa mwaka 2023/24

64. Katika mwaka 2023/24, Serikali inatarajia kukusanya na kutumia jumla ya shilingi bilioni 43,294.6 ikilinganishwa na makadirio ya shilingi bilioni 41,480.6 mwaka 2022/23. Kiasi kilichoongezeka cha shilingi bilioni 1,814.0 ni sawa na asilimia 4.4. Ongezeko hili limezingatia mwenendo halisi wa ukusanyaji wa mapato ya ndani na jitahada zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali za kuongeza mapato. Aidha, ongezeko hilo limezingatia mahitaji yasiyoepukika (first charge expenditure) kama vile mikataba ya kugharamia miradi mbalimbali, deni la Serikali na mishahara ya watumishi wa umma.

4.6 Sera za Mapato na Makadirio katika Muda wa Kati

4.6.1 Hatua za Kuongeza Mapato ya Ndani

65. Katika kusimamia na kuimairisha ukusanyaji wa mapato ya ndani, Serikali itatekeleza hatua zifuatazo:

- (i) Kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini katika sekta za uzalishaji ili kuongeza ushiriki wa sekta binafsi;
- (ii) Kutambua na kusajili biashara zisizo rasmi na zinazoendeshwa kidigitali ili kutanua wigo wa mapato;
- (iii) Kuimarisha usimamizi wa sheria za kodi ili kuongeza ulipaji kodi kwa hiari;
- (iv) Kuimarisha na kuhimiza matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA ya ukusanyaji wa mapato ya ndani; na
- (v) Kudhibiti misamaha ya kodi ili isizidi asilimia moja (1) ya Pato la Taifa.


4.6.2 Makadirio ya Mapato ya Ndani

66. Mapato ya ndani yakijumuisha mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa yanakadiriwa kuongezeka hadi shilingi bilioni 31,034.6 mwaka 2023/24 kutoka makadirio ya shilingi bilioni 28,017.9 mwaka 2022/23. Katika kipindi cha muda wa kati, mapato hayo yanakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 10.3 na kufikia shilingi bilioni 37,642.9 mwaka 2025/26. Mchango wa mapato ya ndani katika bajeti unakadiriwa kuongezeka kutoka asilimia 67.5 mwaka 2022/23 hadi asilimia 72.9 mwaka 2023/24 na kuongezeka hadi asilimia 76.3 mwaka 2025/26.

67. Katika mwaka 2023/24, mapato yanayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (Kodi na Yasiyo ya Kodi) yanakadiriwa kuongezeka kwa asilimia 11.5 hadi shilingi bilioni 26,379.0 kutoka makadirio ya shilingi bilioni 23,652.8 mwaka 2022/23. Katika muda wa kati, mapato hayo yanakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 11.3 hadi shilingi bilioni 32,576.1 mwaka 2025/26. Uwiano wa mapato ya kodi kwa Pato la Taifa ni wastani wa asilimia 12.0 katika kipindi cha muda wa kati. Mchanganuo wa mapato ya ndani ni kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 4.1**.

Kielelezo Na. 4.1: Makadirio ya Mapato ya Ndani katika Muda wa Kati


Shilingi Bilioni



68. Katika muda wa kati, Mapato Yasiyo ya Kodi (Wizara, Idara, Taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa) yanakadiriwa kuongezeka kutoka shilingi bilioni 4,365.1 mwaka 2022/23 hadi shilingi bilioni 4,655.6 mwaka 2023/24 na kuongezeka kufikia shilingi bilioni 5,066.8 mwaka 2025/26. Mapato hayo yanakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 5.1 katika muda wa kati. Mchanganuo wa mapato yasiyo ya kodi ni kama inavyooneshwa katika **Kielelezo Na. 4.2**.

Kielelezo Na. 4.2: Mchanganuo wa Makadirio ya Mapato Yasiyo ya Kodi (Wizara, Idara, Taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa) katika Muda wa Kati

Shilingi Bilioni



69. Katika muda wa kati, Serikali itaendelea kutekeleza mikakati mahsusi ya kisera na kiutawala ili kufikia malengo ya makusanyo ya mapato ya ndani. Mikakati hiyo ni pamoja na:

- (i) Kupanua wigo wa kodi kwa kutekeleza Mkakati wa Ukusanyaji wa Mapato wa Muda wa Kati (2023/24 -2026/27);
- (ii) Kuendelea kuwatengea wafanyabiashara na watoa huduma wadogo maeneo maalum na kuwapatia huduma muhimu za kijamii kwa lengo la kukuza biashara zao pamoja na kutoa fursa kwa wafanyabiashara walio rasmi kulipa kodi stahiki;
- (iii) Kuendelea kutambua na kusajili kampuni za kimataifa zinazoendesha biashara za kidigitali nchini kwa kutumia mfumo wa usajili uliorahisishwa (simplified registration regime);
- (iv) Kuendelea kuwekeza kwenye matumizi ya teknolojia ili kuhakikisha mifumo ya Serikali inabadilishana taarifa;
- (v) Kuendelea na utaratibu wa kuingia makubaliano na walipakodi ili kuwawezesha kulipa madeni yao kwa awamu;
- (vi) Kuendelea kuimarisha ulinzi na usalama kwenye mipaka yote nchini kwa kufanya doria za mara kwa mara ili kudhibiti ukwepaji kodi na biashara za magendo;
- (vii) Kuendelea kutoa elimu ya ulipaji kodi kwa jamii kupitia vyombo vya habari, mitandao ya kijamii, vituo vya huduma kwa walipakodi na kampeni mbalimbali;
- (viii) Kuendelea kusimamia mikakati ya kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya Wizara na Idara Zinazojitegemea;
- (ix) Kuendelea kuhakikisha Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali zinawasilisha Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali gawio na michango stahiki kwa wakati;
- (x) Kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara, Idara Zinazojitegemea na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa lengo la kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato;
- (xi) Kuwajengea uzalendo wananchi ili kujenga msingi wa ulipaji kodi kwa hiari; na
- (xii) Kuandaa na kutekeleza mpango mkakati wa ukusanyaji wa mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

4.7 Sera za Misaada na Makadirio katika Muda wa Kati

4.7.1 Sera za Misaada

70. Serikali itaendelea kutekeleza Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo kwa lengo la kuimarisha majadiliano baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo na kuratibu upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya kusaidia utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali. Aidha, Serikali itatekeleza mikakati ya ushirikiano na

Washirika wa Maendeleo kama ifuatavyo:

- (i) Kuhamasisha Washirika wa Maendeleo kuzingatia matumizi ya mifumo ya Serikali wakati wa utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali;
- (ii) Kuhakikisha fedha za misaada zinaelekezwa kwenye miradi yenye tija na ambayo ni vipaumbele vya Taifa;
- (iii) Kusimamia utaratibu wa kisera wa kutenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya pamoja kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo; na
- (iv) Kusimamia utekelezaji wa makubaliano kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo.

71. Katika mwaka 2023/24, misaada ya Washirika wa Maendeleo inatarajiwa kuwa shilingi bilioni 1,111.3 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1,101.5 mwaka 2022/23 na inatarajiwa kuongezeka na kufikia shilingi bilioni 1,192.2 mwaka 2025/26. Kwa upande wa misaada ya Mifuko ya Pamoja ya Kisekta, kunatarajiwa kuwa na ongezeko na kufikia shilingi bilioni 130.1 kwa mwaka 2023/24 kutoka shilingi bilioni 122.1 mwaka 2022/23 na inatarajiwa kufikia shilingi bilioni 135.0 mwaka 2025/26. Aidha, misaada ya miradi ya maendeleo inakisiwa kuongezeka katika kipindi cha muda wa kati na kufikia shilingi bilioni 1,000.0 kutoka shilingi bilioni 924.8 mwaka 2023/24. Ongezeko hili linatokana na jitihada zinazofanywa na Serikali za kuimarisha mahusiano na nchi marafiki pamoja na mashirika ya fedha ya kimataifa.

4.8 Sera za Matumizi na Makadirio katika Muda wa Kati

4.8.1 Mikakati ya Kusimamia Matumizi

72. Mikakati ya kusimamia matumizi inalenga kuongeza tija na ufanisi pamoja na kuondoa matumizi yasiyo ya lazima kama ifuatavyo:

- (i) Kusimamia nidhamu ya matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia sheria na miongozo;
- (ii) Kuelekeza fedha kwenye maeneo ya kipaumbele ikiwemo sekta za uzalishaji (kilimo, mifugo, uvuvi, madini) hususan kwenye kuongeza thamani ili kuchochea ukuaji wa uchumi na kuhakikisha kuwa miradi inayoendelea inapewa kipaumbele kabla ya kuanza miradi mipya;
- (iii) Kuendelea kusimamia na kutekeleza Mkakati wa Kudhibiti na Kuzuia Malimbikizo ya Madeni ulioboreshwa wa mwaka 2022 ambao unapatikana kwenye Tovuti ya Wizara ya Fedha na Mipango (<https://www.mof.go.tz/publications/revised-strategy-for-management-of-arrears>) pamoja na kutenga bajeti na kulipa madeni yaliyohakikiwa;
- (iv) Kuendelea kuboresha Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma ikiwa ni pamoja na kuweka ukomo wa bei za bidhaa na huduma zinazotumika serikalini ili kudhibiti matumizi ya fedha za Serikali;
- (v) Kuendelea kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika utekelezaji wa shughuli za Serikali ili kubana matumizi ikiwa ni pamoja na kuendesha

vikao kwa njia ya mtandao (virtual meetings) na kuepuka matumizi ya makaratasi;


- (vi) Kuimarisha usimamizi wa miradi kwa kufanya ukaguzi wa ufanisi kwa wakati ili kuokoa gharama za ziada zinazoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wa miradi; na
- (vii) Kudhibiti matumizi ya Serikali kwenye eneo la ununuzi, uendeshaji na matengenezo ya magari.

4.8.2 Makadirio ya Matumizi

73. Katika mwaka 2023/24, matumizi ya Serikali yanakadiriwa kuongezeka kwa asilimia 4.4 kutoka shilingi bilioni 41,480.6 mwaka 2022/23 na kufikia shilingi bilioni 43,294.6 sawa na asilimia 20.7 ya Pato la Taifa. Ongezeko hili limechangiwa na ukuaji wa mahitaji ya: Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ikijumuisha ulipaji wa deni la Serikali; kugharamia mishahara ya Watumishi wa Umma; pamoja na kugharamia miradi ya kielelezo inayoendelea. Katika muda wa kati, matumizi ya Serikali yanakadiriwa kuongezeka kwa wastani wa asilimia 6.9 kwa mwaka hadi shilingi bilioni 50,154.2 mwaka 2025/26. **Kielelezo Na. 4.3** kinaonesha makadirio ya matumizi katika muda wa kati.

Kielelezo Na. 4.3: Mwenendo wa Makadirio ya Matumizi katika Muda wa Kati

Shilingi Bilioni




74. Katika mwaka 2023/24, matumizi ya kawaida yanakadiriwa kufikia shilingi bilioni 28,266.6 kutoka makadirio ya shilingi bilioni 26,474.6 mwaka 2022/23, sawa na ongezeko la asilimia 6.8. Makadirio haya ni sawa na asilimia 13.5 ya Pato la Taifa. Kati ya kiasi hicho, gharama za kuhudumia Deni la Serikali ikijumuisha gharama nyingine za Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali (CFS Others) zinakadiriwa kufikia shilingi bilioni 12,488.2 mwaka 2023/24 kutoka makadirio ya shilingi bilioni 11,308.4 mwaka 2022/23 na Mishahara kwa Watumishi wa Umma inakadiriwa kuongezeka hadi shilingi bilioni 10,251.3 mwaka 2023/24 kutoka makadirio ya shilingi bilioni

9,830.8 mwaka 2022/23, sawa na ongezeko la asilimia 4.3. Ongezeko hili linatokana na upandishwaji vyeo pamoja na ajira mpya hususan katika sekta za afya na elimu. Matumizi Mengineyo yanakadiriwa kuwa shilingi bilioni 5,527.1 mwaka 2023/24 ikilinganishwa na shilingi bilioni 5,335.5 mwaka 2022/23. Ongezeko hili linachangiwa na ugharamiaji wa uendeshaji wa miradi ya maendeleo iliyokamilika.

75. Matumizi ya maendeleo yanakadiriwa kuwa shilingi bilioni 15,028.0 mwaka 2023/24 kutoka shilingi bilioni 15,006.0 mwaka 2022/23 na kuongezeka kwa wastani wa asilimia 5.9 kwa mwaka hadi shilingi bilioni 17,778.1 mwaka 2025/26. Bajeti ya matumizi ya maendeleo kwa mwaka 2023/24 ni sawa na asilimia 34.7 ya bajeti yote. Hii imetokana na kuongezeka kwa mahitaji ya uendeshaji katika matumizi ya kawaida ikiwemo deni la Serikali; mishahara ya watumishi wa umma; uendeshaji wa miradi iliyokamilika ikijumuisha miundombinu ya kutolea huduma za afya na elimu; maandalizi ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2024; na maandalizi ya Dira Mpya ya Taifa ya Maendeleo mwaka 2050. Aidha, kufuatia matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, ni dhahiri kuwa gharama za utoaji huduma za jamii zitaongezeka kutokana na ongezeko la idadi ya watu nchini kutoka watu 44,928,923 mwaka 2012 hadi watu 61,741,120 mwaka 2022. Kati ya fedha za matumizi ya maendeleo, shilingi bilioni 11,745.9 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 3,282.1 ni fedha za nje. Mgawanyo wa matumizi ya kawaida na maendeleo ni kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 4.4**.

Kielelezo Na. 4.4 Makadirio ya Aina Kuu za Matumizi



4.8.3 Makadirio ya Matumizi Kisekta


76. Matumizi ya kisekta yamegawanyika katika sehemu saba kwa kuzingatia majukumu na shughuli za Serikali. Sekta hizo ni pamoja na: Huduma za Utawala na Deni la Serikali; Maendeleo ya Uchumi; Elimu; Ulinzi, Sheria, na Usalama; Afya; Hifadhi ya Jamii; na Maji, Makazi na Maendeleo ya Jamii.

77. Katika muda wa kati, makadirio ya matumizi katika sekta ya Huduma za Utawala na Deni la Serikali yanakadiriwa kuongezeka kutoka shilingi bilioni 16,797.4 mwaka 2022/23 hadi shilingi bilioni 18,066.9 mwaka 2023/24 na kuendelea kuongezeka kufikia shilingi bilioni 21,485.6 mwaka 2025/26. Aidha, makadirio ya matumizi katika sekta ya Maendeleo ya Uchumi yanakadiriwa kuongezeka kutoka shilingi bilioni 9,064.2 mwaka 2022/23 hadi shilingi bilioni 9,264.1 mwaka 2023/24 na kuendelea kuongezeka kufikia shilingi bilioni 10,527.7 mwaka 2025/26. Vile vile, matumizi katika sekta ya Elimu yanakadiriwa kuongezeka kutoka shilingi bilioni 5,684.6 mwaka 2022/23 hadi shilingi bilioni 5,810.0 mwaka 2023/24 na kuendelea kuongezeka kufikia shilingi bilioni 6,602.4 mwaka 2025/26.

78. Matumizi katika sekta ya Ulinzi, Sheria na Usalama yanakadiriwa kuongezeka kutoka shilingi bilioni 4,208.0 mwaka 2022/23 hadi shilingi bilioni 4,300.8 mwaka 2023/24 na kuendelea kuongezeka kufikia shilingi bilioni 4,887.4 mwaka 2025/26. Matumizi katika sekta ya Afya yanakadiriwa kuongezeka kutoka shilingi bilioni 2,149.1 mwaka 2022/23 hadi shilingi bilioni 2,196.6 mwaka 2023/24 na kuongezeka kufikia shilingi bilioni 2,496.2 mwaka 2025/26. Matumizi katika sekta ya Hifadhi ya Jamii yanakadiriwa kuongezeka kutoka shilingi bilioni 2,244.2 mwaka 2022/23 hadi shilingi bilioni 2,293.8 mwaka 2023/24 na kuongezeka kufikia shilingi bilioni 2,606.6 mwaka 2025/26. Matumizi katika sekta ya Maji, Makazi na Maendeleo ya Jamii yanakadiriwa kuongezeka kutoka shilingi bilioni 1,333.1 mwaka 2022/23 hadi shilingi bilioni 1,362.5 mwaka 2023/24 na kuongezeka kufikia shilingi bilioni 1,548.3 mwaka 2025/26. Mgawanyo wa makadirio kwa kila sekta umeoneshwa kwenye **Kielelezo Na. 4.6 na Jedwali Na. 4.5.**

Kielelezo Na. 4.6: Uainishaji wa Makadirio ya Matumizi Kisekta

Shilingi Bilioni



4.9 Ugharamiaji wa Nakisi ya Bajeti

79. Serikali itaendelea kugharamia nakisi ya bajeti kwa kutumia fursa ya kupata mikopo nafuu kutoka vyanzo vya ndani na nje ili kutoathiri uhimilivu wa deni la Serikali. Kipaumbele kikubwa cha mikopo kutoka nje kitakuwa mikopo yenye masharti nafuu kama ilivyoainishwa katika Mkakati wa Muda wa Kati wa Kusimamia Deni la Serikali na mikopo yenye masharti ya kibiashara itakopwa kwa ajili ya kugharamia miradi inayochochea kasi ya ukuaji wa uchumi. Ukopaji katika vyanzo vya ndani utalenga kugharamia bajeti pamoja na kuendeleza soko la ndani la dhamana za Serikali.

4.9.1 Ukopaji kutoka Vyanzo vya Ndani

80. Serikali itaendelea kukopa katika soko la ndani la dhamana za Serikali ili kugharamia miradi ya maendeleo bila kuathiri upatikanaji wa mikopo kwa sekta binafsi. Aidha, Serikali itaendelea na jitihada za kukuza na kuendeleza soko la ndani la dhamana za Serikali kwa kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na: Kupanua wigo wa wawekezaji kwa kutoa elimu kuhusu faida za kuwekeza katika soko la ndani na kuweka mazingira wezeshi na shindani kwa wawekezaji kutoka nchi wanachama wa EAC, SADC na watanzania waishio nje ya nchi. Katika mwaka 2023/24, Serikali inatarajia kukopa shilingi bilioni 5,638.5 ambapo shilingi bilioni 3,542.1 ni kwa ajili ya kulipia mikopo itakayoiva na shilingi bilioni 2,096.4 (sawa na asilimia moja (1) ya Pato la Taifa) ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo

4.9.2 Ukopaji kutoka Vyanzo vya Nje

81. Katika mwaka 2023/24, Serikali inatarajia kukopa shilingi bilioni 5,510.2 kutoka vyanzo vya nje. Kati ya hizo, mikopo yenye masharti nafuu ni shilingi bilioni 3,399.7 na mikopo yenye masharti ya kibiashara ni shilingi bilioni 2,110.5. Katika kipindi cha muda wa kati, Serikali inatarajia kukopa wastani wa shilingi bilioni 5,017.1 kwa mwaka.

4.10 Sura ya Bajeti

82. Sura ya bajeti katika kipindi cha muda wa kati 2022/23 – 2025/26 ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 4.1 hadi 4.5.**

Jedwali Na. 4.1: Makadirio ya Bajeti katika Kipindi cha Muda wa Kati 2022/23 - 2025/26 (Analytical Budget Frame)

Shilingi Bilioni

	2022/23 BAJETI ILIYODHINISHWA	2023/24 MAKADIRIO YA BAJETI	2024/25 MAKADIRIO YA BAJETI	2025/26 MAKADIRIO YA BAJETI
Mapato ya Ndani (Ikijumuisha Mapato ya Halmashauri)	28,017.9	31,034.6	34,079.7	37,642.9
Mapato ya Ndani	27,005.6	29,890.7	32,867.2	36,353.5
Mapato ya TRA (Kodi na Yasiyo Ya Kodi)	23,652.8	26,379.0	29,247.6	32,576.1
Mapato Yasiyo ya Kodi (Wizara, Taasisi na Mashirika)	3,352.8	3,511.7	3,619.6	3,777.4
Mapato ya Halmashauri	1,012.3	1,143.9	1,212.5	1,289.4
Jumla ya Matumizi	35,264.5	37,084.3	39,215.8	42,258.0
Matumizi ya Kawaida	20,258.5	22,056.3	23,304.6	24,479.9
Malipo ya Riba Nje	1,100.8	1,239.3	1,384.6	1,440.2
Malipo ya Riba Ndani	1,770.2	2,736.9	3,013.0	3,193.8
Mishahara	9,830.8	10,251.3	10,672.1	11,187.6
Michango ya Serikali kwenye Mifuko ya Jamii	1,655.7	1,710.6	1,872.3	2,050.8
Bidhaa/ Huduma/ Ruzuku	7,112.3	7,414.2	7,679.8	8,006.7
o/w Matumizi Mengineyo	4,068.0	4,179.3	4,358.2	4,547.8
Matumizi ya Maendeleo	15,006.0	15,028.0	15,911.1	17,778.1
Fedha za Ndani	12,306.9	11,745.9	12,826.4	14,589.5
Fedha za Nje	2,699.1	3,282.1	3,084.8	3,188.6
Nakisi ya Bajeti bila ya Kujumlisha Misaada	(7,246.7)	(6,049.7)	(5,136.0)	(4,615.1)
Misaada	1,101.5	1,111.3	1,117.2	1,192.2
Misaada ya Kibajeti	55.5	56.4	57.2	57.2
Misaada ya Maendeleo	923.8	924.8	927.8	1,000.0
Mifuko ya Kisekta	122.1	130.1	132.1	135.0
Nakisi ya Bajeti Ikijumuisha Misaada	(6,145.2)	(4,938.4)	(4,018.9)	(3,422.9)
Jumla ya Nakisi	(6,145.2)	(4,938.4)	(4,018.9)	(3,422.9)
Kuziba Nakisi	6,145.2	4,938.4	4,018.9	3,422.9
Kuziba Nakisi Kutoka Nje	3,665.0	2,842.0	1,919.5	1,344.2
Mikopo Nafuu ya Kibajeti	1,893.9	1,172.5	712.2	474.8
Mikopo Nafuu ya Miradi ya Maendeleo	1,653.1	2,227.1	2,024.8	2,053.6
Mikopo Nafuu ya Mifuko ya Kisekta	0.0	0.0	0.0	0.0
Mikopo ya Kibiashara	3,034.0	2,110.6	2,136.7	2,138.9
Malipo ya Mtaji Deni la Nje	(2,916.0)	(2,668.3)	(2,954.3)	(3,323.1)
Kuziba Nakisi Kutoka Ndani	2,480.1	2,096.4	2,099.4	2,078.6
Malipo ya Mtaji Deni la Ndani (Rollover)	3,300.0	3,542.1	3,663.7	4,573.2
Malipo ya Mtaji Deni la Ndani (Rollover)	(3,300.0)	(3,542.1)	(3,663.7)	(4,573.2)
Pato Ghafi la Taifa	188,202.8	209,642.4	233,261.8	259,828.7

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

Jedwali Na. 4.2: Makadirio ya Bajeti kwa Asilimia ya Pato Ghafi la Taifa kwa Kipindi cha Muda wa Kati 2022/23 -2024/25

	2022/23 BAJETI ILIYOIDHINISHWA	2023/24 MAKADIRIO YA BAJETI	2024/25 MAKADIRIO YA BAJETI	2025/26 MAKADIRIO YA BAJETI
Mapato ya Ndani (Ikijumuisha Mapato ya Halmashauri)	14.9%	14.8%	14.6%	14.5%
Mapato ya Ndani	14.3%	14.3%	14.1%	14.0%
Mapato ya TRA (Kodi na Yasiyo Ya Kodi)	12.6%	12.6%	12.5%	12.5%
Mapato Yasiyo ya Kodi (Wizara, Taasisi na Mashirika)	1.8%	1.7%	1.6%	1.5%
Mapato ya Halmashauri	0.5%	0.5%	0.5%	0.5%
Jumla ya Matumizi	18.7%	17.7%	16.8%	16.3%
Matumizi ya Kawaida	10.8%	10.5%	10.0%	9.4%
Malipo ya Riba Nje	0.6%	0.6%	0.6%	0.6%
Malipo ya Riba Ndani	0.9%	1.3%	1.3%	1.2%
Mishahara	5.2%	4.9%	4.6%	4.3%
Michango ya Serikali kwenye Mifuko ya Jamii	0.9%	0.8%	0.8%	0.8%
Bidhaa/ Huduma/ Ruzuku	3.8%	3.5%	3.3%	3.1%
o/w Matumizi Mengineyo	2.2%	2.0%	1.9%	1.8%
Matumizi ya Maendeleo	8.0%	7.2%	6.8%	6.8%
Fedha za Ndani	6.5%	5.6%	5.5%	5.6%
Fedha za Nje	1.4%	1.6%	1.3%	1.2%
Nakisi ya Bajeti bila ya Kujumlisha Misaada	-3.9%	-2.9%	-2.2%	-1.8%
Misaada	0.6%	0.5%	0.5%	0.5%
Misaada ya Kibajeti	0.0%	0.0%	0.0%	0.0%
Misaada ya Maendeleo	0.5%	0.4%	0.4%	0.4%
Mifuko ya Kisekta	0.1%	0.1%	0.1%	0.1%
Nakisi ya Bajeti Ikijumuisha Misaada	-3.3%	-2.4%	-1.7%	-1.3%
Jumla ya Nakisi	-3.3%	-2.4%	-1.7%	-1.3%
Kuziba Nakisi	3.3%	2.4%	1.7%	1.3%
Kuziba Nakisi Kutoka Nje	1.9%	1.4%	0.8%	0.5%
Mikopo Nafuu ya Kibajeti	1.0%	0.6%	0.3%	0.2%
Mikopo Nafuu ya Miradi ya Maendeleo	0.9%	1.1%	0.9%	0.8%
Mikopo Nafuu ya Mifuko ya Kisekta	0.0%	0.0%	0.0%	0.0%
Mikopo ya Kibiashara	1.6%	1.0%	0.9%	0.8%
Kulipa Mtaji Deni la Nje	-1.5%	-1.3%	-1.3%	-1.3%
Kuziba Nakisi Kutoka Ndani	1.3%	1.0%	0.9%	0.8%
Kulipa Mtaji Deni la Ndani (Rollover)	1.8%	1.7%	1.6%	1.8%
Kulipa Mtaji Deni la Ndani (Rollover)	-1.8%	-1.7%	-1.6%	-1.8%

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

Jedwali Na. 4.3: Makadirio ya Bajeti katika Kipindi cha Muda wa Kati 2022/23 - 2025/26 (Accounting Budget Frame)

Shilingi Bilioni

	2022/23 BAJETI ILYOIDHINISHWA	2023/24 MAKADIRIO YA BAJETI	2024/25 MAKADIRIO YA BAJETI	2025/26 MAKADIRIO YA BAJETI
I. JUMLA YA MAPATO	41,480.6	43,294.6	45,833.8	50,154.2
Mapato ya Ndani (ikijumuisha Mapato ya Halmashauri)	28,017.9	31,034.6	34,079.7	37,642.9
Mapato ya Ndani	27,005.6	30,490.7	34,267.2	38,503.5
Mapato ya Halmashauri	1,012.3	1,143.9	1,282.5	1,439.4
Misaada na Mikopo Nafuu ya Kibajeti	1,949.5	1,228.9	769.5	532.0
Misaada na Mikopo Nafuu ya Miradi	2,577.0	3,152.0	2,952.7	3,053.6
Mifuko ya Kisekta	122.1	130.1	132.1	135.0
Kulipa Mtaji Deni la Ndani (Rollover)	3,300.0	3,542.1	3,663.7	4,573.2
Mikopo ya Ndani ya Kibiashara	2,480.1	2,096.4	2,099.4	2,078.6
Mikopo ya Nje ya Kibiashara	3,034.0	2,110.6	2,136.7	2,138.9
II. JUMLA YA MATUMIZI	41,480.6	43,294.6	45,833.8	50,154.2
MATUMIZI YA KAWAIDA	26,474.6	28,266.6	29,922.6	32,376.1
Mfuko Mkuu wa Serikali	11,308.4	12,488.2	13,502.7	15,199.3
Mishahara	9,830.8	10,251.3	10,672.1	11,187.6
Matumizi Mengineyo	5,335.5	5,527.1	5,747.8	5,989.3
MATUMIZI YA MAENDELEO	15,006.0	15,028.0	15,911.1	17,778.1
Fedha za Ndani	12,306.9	11,745.9	12,826.4	14,589.5
Fedha za Nje	2,699.1	3,282.1	3,084.8	3,188.6
Pato Ghafi la Taifa	188,202.8	209,642.4	233,261.8	259,828.7

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

Jedwali Na. 4.4: Makadirio ya Bajeti kwa Asilimia ya Pato la Taifa kwa Kipindi cha Muda wa Kati 2022/23 -2025/26

	2022/23 BAJETI ILIYOJDHINISHWA	2023/24 MAKADIRIO YA BAJETI	2024/25 MAKADIRIO YA BAJETI	2025/26 MAKADIRIO YA BAJETI
I. JUMLA YA MAPATO	22.0%	20.7%	19.6%	19.3%
Mapato ya Ndani (ikijumuisha Mapato ya Halmashauri)	14.9%	14.8%	14.6%	14.5%
Mapato ya Ndani	14.3%	14.5%	14.7%	14.8%
Mapato ya Halmashauri	0.5%	0.5%	0.5%	0.6%
Misaada na Mikopo Nafuu ya Kibajeti	1.0%	0.6%	0.3%	0.2%
Misaada na Mikopo Nafuu ya Miradi	1.4%	1.5%	1.3%	1.2%
Mifuko ya Kisekta	0.1%	0.1%	0.1%	0.1%
Kulipa Mtaji Deni la Ndani (Rollover)	1.8%	1.7%	1.6%	1.8%
Mikopo ya Ndani ya Kibiashara	1.3%	1.0%	0.9%	0.8%
Mikopo ya Nje ya Kibiashara	1.6%	1.0%	0.9%	0.8%
II. JUMLA YA MATUMIZI	22.0%	20.7%	19.6%	19.3%
MATUMIZI YA KAWAIDA	14.1%	13.5%	12.8%	12.5%
Mfuko Mkuu wa Serikali	6.0%	6.0%	5.8%	5.8%
Mishahara	5.2%	4.9%	4.6%	4.3%
Matumizi Mengineyo	2.8%	2.6%	2.5%	2.3%
MATUMIZI YA MAENDELEO	8.0%	7.2%	6.8%	6.8%
Fedha za Ndani	6.5%	5.6%	5.5%	5.6%
Fedha za Nje	1.4%	1.6%	1.3%	1.2%

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

**Jedwali Na. 4.5: Makadirio ya Bajeti Kisekta katika Kipindi cha Muda wa Kati
2022/23 -2025/26**

Shilingi Bilioni

SEKTA	NAMBA YA SEKTA	2022/23 BAJETI ILIYOIDHINISHWA	2023/24 MAKADIRIO YA BAJETI	2024/25 MAKADIRIO YA BAJETI	2025/26 MAKADIRIO YA BAJETI
1 - Elimu	709	5,684.6	5,810.0	6,110.1	6,602.4
1.1 - Elimu Msingi	7091,7092	4,368.3	4,464.6	4,695.2	5,073.6
1.2 - Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi	7,093	145.0	148.2	155.9	168.4
1.3 - Elimu ya Juu	7,094	1,006.4	1,028.6	1,081.7	1,168.9
1.4 - Sayansi, Teknolojia na Ubunifu	7,098	67.0	68.5	72.0	77.8
1.5 - Huduma za Utawala	7,098	97.9	100.1	105.2	113.7
2 - Afya	707	2,149.1	2,196.6	2,310.0	2,496.2
2.1 - Huduma za Tiba	7071,7072,7073,7074,7075,7076	862.0	881.0	926.5	1,001.2
2.2 - Huduma za Kinga	7071,7073,7074,7076	258.4	264.1	277.8	300.1
2.3 - Hospitali za Rufaa za Mikoa	7071,7072,7073,7074	1.0	1.1	1.1	1.2
2.4 - Zahanati	7071,7072,7073,7074,7075	96.6	98.7	103.8	112.2
2.5 - Vituo vya Afya	7071,7072,7073,7074,7075	153.8	157.1	165.3	178.6
2.6 - Hospitali za Wilaya	7071,7072,7073,7074,7075	691.5	706.8	743.3	803.2
2.7 - Huduma za Utawala	7,076	85.9	87.8	92.3	99.7
3 - Huduma za Utawala na Deni la Serikali	701	16,797.4	18,066.9	19,303.0	21,485.6
3.1 - Mihimili	7,011	3,809.3	3,893.3	4,094.4	4,424.4
3.2 - Usimamizi wa mapato na Matumizi	7,011	3,693.0	3,774.5	3,969.5	4,289.3
3.3 - Mambo ya Nje na Ushirikano wa Kimataifa	7,011	208.0	212.6	223.6	241.6
3.4 - Deni la Serikali	7,018	9,087.0	10,186.5	11,015.6	12,530.3
4 - Ulinzi, Utawala wa Sheria na Usalama	703	4,208.0	4,300.8	4,523.0	4,887.4
4.1 - Ulinzi	702	2,712.0	2,771.9	2,915.0	3,149.9
4.2 - Usalama wa Umma	7,036	1,206.2	1,232.8	1,296.5	1,401.0
4.3 - Mahakama	7,033	289.7	296.1	311.4	336.5
5 - Maendeleo ya Uchumi	704	9,064.2	9,264.1	9,742.6	10,527.7
5.1 - Kilimo	7,042	1,216.2	1,243.0	1,307.2	1,412.5
5.2 - Madini	7,044	83.3	85.2	89.6	96.8
5.3 - Nishati	7,043	2,905.9	2,970.0	3,123.4	3,375.1
5.4 - Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano	7045, 7046	3,929.2	4,015.8	4,223.2	4,563.6
5.5 - Maliasili, Utalii na Mazingira	7,049	615.4	629.0	661.5	714.8
5.6 - Viwanda	7,047	99.1	101.3	106.5	115.1
5.7 - Biashara	7,047	183.8	187.9	197.6	213.5
5.8 - Kazi, Maendeleo ya Vijana na Kukuza Ujuzi	7,041	31.2	31.9	33.6	36.3
6 - Hifadhi ya Jamii	710	2,244.2	2,293.8	2,412.2	2,606.6
6.1 - Wazee, Watoto na Watu wenye Ulemavu	7101,7102	37.3	38.1	40.1	43.3
6.2 - Mifuko ya Hifadhi ya Jamii	7,109	1,761.1	1,800.0	1,893.0	2,045.5
6.3 - Mfuko wa Bima wa Afya	7,109	445.9	455.7	479.2	517.8
7 - Maji, Makazi na Maendeleo ya Jamii	706	1,333.1	1,362.5	1,432.8	1,548.3
7.1 - Maji	7,063	723.8	739.8	778.0	840.7
7.2 - Ardhi, Nyumba na Makazi ya Watu	7,065	118.6	121.2	127.4	137.7
7.3 - Maendeleo ya Jamii	7,062	455.2	465.3	489.3	528.7
7.4 - Habari, Michezo na Utamaduni	7,081	35.4	36.2	38.1	41.1
Jumla		41,480.6	43,294.6	45,833.8	50,154.2

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

SURA YA TANO
VIHATARISHI VYA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI PAMOJA NA
MIKAKATI YA KUKABILIANA NAVYO

5.1 Utangulizi

83. Vihatarishi ni matukio yasiyotarajiwa ambayo yanaweza kuathiri utekelezaji wa mpango na bajeti. Sura hii inaainisha vihatarishi vinavyoweza kujitokeza na kuathiri utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2023/24. Aidha, hatua za kubainisha na kukabiliana na vihatarishi zimeainishwa kwa kuzingatia Mwongozo wa Taifa wa Kuandaa na Kusimamia Mpango wa Usimamizi wa Vihatarishi katika Taasisi za Umma wa Mwaka 2012 na Kifungu Na. 4 (2) (c) pamoja na Kanuni ya 4 (1) na (2) ya Sheria ya Bajeti, Sura 439.

5.2 Vihatarishi vya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali

84. Vihatarishi katika utekelezaji wa mpango na bajeti vinaweza kusababishwa na mabadiliko ya: tabianchi, hali ya soko, uongozi wa kisiasa, sera, ushindani, mfumo wa uratibu na usimamizi pamoja na teknolojia katika uzalishaji na usambazaji wa bidhaa na huduma. Matokeo ya mabadiliko hayo yanaweza kuathiri mwenendo wa viashiria vya uchumi jumla na utekelezaji wa mpango na bajeti hususan, malengo ya ukusanyaji wa mapato na gharama za matumizi. Hivyo, vihatarishi vinavyoweza kuathiri utekelezaji wa mpango na bajeti ya Serikali kwa mwaka 2023/24 ni pamoja na:

- (i) Mfumuko wa bei;
- (ii) Viwango vya kubadilisha fedha;
- (iii) Ukuaji wa Pato la Taifa; na
- (iv) Viwango vya riba katika soko la fedha la ndani na nje.
- (v) Mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa mazingira;
- (vi) Majanga asilia kama vile matetemeko ya ardhi, ukame, mafuriko na magonjwa ya mlipuko;
- (vii) Mabadiliko ya sera za kibajeti, mikopo na misaada;
- (viii) Ubadhirifu wa fedha na mali za umma; na
- (ix) Madeni sanjari (contingent liabilities).

5.3 Athari za vihatarishi katika utekelezaji wa mpango na bajeti

85. Athari zinazoweza kujitokeza endapo vihatarishi vya mwenendo wa uchumi jumla na utekelezaji wa bajeti vitatokea ni pamoja na:

- (i) Kuongezeka kwa nakisi ya bajeti;
- (ii) Kutokufikiwa kwa lengo la ukusanyaji wa mapato;
- (iii) Kuongezeka kwa bei za bidhaa na huduma sambamba na kupungua kwa uzalishaji viwandani na mashambani kulikosababishwa na changamoto ya upatikanaji wa malighafi muhimu za viwandani na kilimo kama vile ngano, mbolea na mafuta ghafi kutokana na vita inayoendelea nchini Ukraine;

- (iv) Kasi ndogo ya utekelezaji wa miradi;
- (v) Kuongezeka kwa gharama za bidhaa, malighafi, huduma na utekelezaji wa miradi;
- (vi) Kuongezeka kwa gharama za kuhudumia deni la Serikali;
- (vii) Kuongezeka kwa gharama za mikopo ya kibiashara katika masoko ya fedha;
- (viii) Kupungua kwa misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo;
- (ix) Kutopatikana kwa thamani halisi ya fedha katika miradi ya maendeleo kutokana na kutekelezwa pasipo kuzingatia ubora;
- (x) Kuongezeka kwa madai na madeni ya wazabuni na watoa huduma; na
- (xi) Kuongezeka kwa Deni la Serikali.

5.4 Hatua za kukabiliana na vihatarishi

86. Ili kufikia malengo na shabaha za utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2023/24, Serikali itaendelea na mikakati na hatua za kukabiliana na vihatarishi vinavyoweza kujitokeza, ikiwa ni pamoja na:

- (i) Kusimamia miongozo ya kubaini vihatarishi katika uendelezaji wa shughuli za kiuchumi ili kuchukua hatua stahiki za kisera na kiutawala kabla, wakati na baada ya kutokea;
- (ii) Kuimarisha uwezo wa Serikali katika kupambana na vitendo vya ukwepaji kodi ikiwemo uboreshaji wa mifumo ya TEHAMA, udhibiti wa biashara za magendo, utoaji wa elimu kwa mlipakodi pamoja na kupanua wigo wa ukusanyaji wa mapato;
- (iii) Kutoa unafuu wa upatikanaji wa pembejeo ikiwemo mbolea, zana za kilimo, viuatilifu, mbegu bora na kuimarisha kilimo cha umwagiliaji. Katika kuongeza uzalishaji na upatikanaji wa mbolea nchini, Serikali inaendelea kutoa ruzuku ya mbolea na kuvipa kipaumbele viwanda vya ndani vya mbolea katika matumizi ya chokaa ili kupunguza gharama za uzalishaji. Aidha, katika bajeti ya mwaka 2022/23, Serikali ilitenga ruzuku ya shilingi bilioni 500.0 kwa ajili ya kutoa ruzuku ya mafuta ya petroli;
- (iv) Kuimarisha usimamizi na udhibiti wa matumizi ya Serikali;
- (v) Kusimamia sera za fedha na bajeti kwa weledi ili kufikia malengo na shabaha za kiuchumi ikiwemo kudhibiti mzunguko wa fedha kulingana na mahitaji ya shughuli za kiuchumi;
- (vi) Kuboresha mazingira ya uwekezaji, upanuzi wa biashara, uzalishaji pamoja na uuzaji wa bidhaa na huduma nje ya nchi;
- (vii) Kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji na tathmini katika ngazi na taasisi zote za umma ili kuwezesha maamuzi ya kiutendaji kufanyika kwa wakati;
- (viii) Kuimarisha ukaguzi wa papo kwa papo (real time audit) ili kuipa taasisi uwezo wa kubaini changamoto katika utekelezaji mapema na kuchukua hatua stahiki kupunguza athari hasi katika utekelezaji wa mpango na bajeti;

- (ix) Kuimarisha usalama wa chakula na upatikanaji wa bidhaa muhimu ikiwemo petroli;
- (x) Kuimarisha utawala bora;
- (xi) Kuimarisha mfuko wa taifa wa maafa;
- (xii) Kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali na nchi rafiki pamoja na mashirika ya Kimataifa;
- (xiii) Kuandaa mpango na bajeti kwa kuzingatia taarifa za Taasisi na Mashirika ya Umma kuhusu mwenendo wa mashauri yaliyopo mahakamani, dhamana chechefu na madai mbalimbali;
- (xiv) Kujenga uwezo wa jamii katika kukabiliana na kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi; kutekeleza lengo la upandaji miti milioni 1.5 kwa kila halmashauri kwa kila mwaka; kulinda na kuhifadhi vyanzo vya maji; kuboresha usimamizi wa taka; kuzuia kuenea kwa viumbe vamizi; na kuboresha mazingira endelevu ya mijini; na
- (xv) Kuendelea kusimamia Deni la Serikali kwa weledi.

SEHEMU YA PILI

**MAELEKEZO YA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA
FEDHA 2023/24**

SURA YA KWANZA
MAELEKEZO YA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA
2023/24

1.1. Utangulizi

87. Sura hii inatoa maelekezo mahsusi yanayopaswa kuzingatiwa na Maafisa Masuuli wakati wa uandaaji, uwasilishaji, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini pamoja na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2023/24.

1.2. Uandaaji wa Mpango na Bajeti

88. Wakati wa kuandaa Mpango na Bajeti, Maafisa Masuuli wanapaswa kuzingatia vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/24, Sera na Miongozo mbalimbali pamoja na Mpango Mkakati wa taasisi husika. Aidha, wanapaswa kufanya mapitio ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2021/22, mapitio ya nusu mwaka 2022/23 na kuandaa mikakati ya kukabiliana na changamoto zilizojitokeza.

89. Maafisa Masuuli wanapaswa kuzingatia viwango vya ukomo wa bajeti vinavyotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya mishahara, matumizi mengineyo na maendeleo. Aidha, kwa Taasisi na Mashirika ya Umma ambayo hayapokei ruzuku kutoka Wizara ya Fedha na Mipango yanapaswa kuzingatia ukomo wa bajeti unaopitishwa na Bodi za Taasisi na Mashirika husika pamoja na maelekezo mahsusi ya Ofisi ya Msajili wa Hazina.

1.3. Kamati za Bajeti

90. Katika maandalizi na utekelezaji wa Bajeti za Mafungu kwa mwaka 2023/24, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuhakikisha kuwa:

- (i) Kamati za Bajeti zinaundwa na zinafanya kazi kwa mujibu wa Kifungu 18(2) cha Sheria ya Bajeti Sura 439; na
- (ii) Muhtasari wa vikao vya kila mwezi vya Kamati za Bajeti kuhusu ugawaji wa rasilimali fedha zinazopokelewa/zinazokusanywa inawasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango kila robo mwaka ambapo Taasisi na Mashirika ya Umma zitawasilisha kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina na Mamlaka za Serikali za Mitaa zitawasilishwa kupitia OR - TAMISEMI kwa ajili ya ukaguzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

1.4. Ukusanyaji wa Mapato

91. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali kwa kusimamia kikamilifu Sera za Mapato zilizopitishwa na Serikali. Katika kutekeleza hayo,

Maafisa Masuuli wanaelekezwa yafuatayo:

- (i) Kushirikiana na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia katika utoaji wa elimu ya ulipaji kodi, tozo na ada kwa hiari ili kuongeza uzalendo kwa wananchi kuchangia maendeleo;
- (ii) Kuhakikisha kuwa mapato yote yanayokusanywa yanaingizwa kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa wakati isipokuwa pale ilipoelekezwa vinginevyo kwa mujibu wa Sheria husika;
- (iii) Kuimarisha taratibu za ukusanyaji na udhibiti wa upotevu wa mapato ya Serikali kwa kutumia Mfumo wa Serikali wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato (GePG) na kuzingatia Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348 inayoelekeza taasisi zote za Serikali kutumia Mfumo wa GePG na kutumia Namba ya kumbukumbu ya malipo;
- (iv) Kuhakikisha Taasisi zote za Serikali zinatumia Mfumo wa Serikali wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato (GePG);
- (v) Kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato;
- (vi) Kuzingatia Sheria za Kodi ikiwa ni pamoja na kukata kodi ya zuio (withholding tax) na kudai risiti za kielektroniki kwa malipo yote yanayofanywa kwa wazabuni na wakandarasi;
- (vii) Kuwasilisha kila mwezi Wizara ya Fedha na Mipango taarifa za makusanyo kutoka kila chanzo. Aidha, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapaswa kuwasilisha OR - TAMISEMI taarifa za makusanyo ya mapato ya ndani ifikapo tarehe 10 ya kila mwezi. Vile vile OR - TAMISEMI iwasilishe taarifa za makusanyo za kila mwezi Wizara ya Fedha na Mipango ifikapo tarehe 15 ya kila mwezi;
- (viii) Kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango mapendekezo ya mabadiliko ya viwango vya kodi, ushuru na tozo mbalimbali ifikapo Novemba kila mwaka;
- (ix) Kuendelea kujenga uwezo wa viongozi na watendaji wanaohusika na ukusanyaji wa mapato ili kuwa na uelewa juu ya utambuzi wa fursa na uibuaji wa vyanzo vipya vya mapato;
- (x) Kuimarisha ushirikiano na mashirika ya umma na Taasisi za Serikali zinazofanya biashara na wakandarasi wanaopewa kazi na Taasisi hizo ili kuziwezesha Halmashauri kukusanya ushuru wa huduma bila vikwazo;
- (xi) Kusimamia utekelezaji wa mkataba uliowekwa na Serikali kati ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mamlaka ya Mapato Tanzania kuhusu utoaji wa takwimu za wafanyabiashara ili kuwezesha Halmashauri kupata taarifa muhimu za ukusanyaji wa ushuru wa huduma;
- (xii) OR - TAMISEMI na Sekretariati za Mikoa kuzisimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa katika ukusanyaji wa mapato;
- (xiii) Mamlaka za Serikali za Mitaa ziendeele kufunga Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi na Uendeshaji wa Vituo vya Kutolea Huduma za Afya Tanzania

- (GoT - HoMIS) kwa ajili ya kusimamia takwimu za huduma na kudhibiti ukusanyaji wa mapato kwenye vituo vya kutolea huduma za afya;
- (xiv) Kuimarisha mifumo ya usimamizi katika Mashirika, Taasisi za Umma, Wakala wa Serikali, na Kampuni ambazo Serikali ina hisa ili kuongeza ufanisi na kuhakikisha gawio na michango stahiki inawasilishwa kwa wakati;
 - (xv) Kufanya tathmini ya mwenendo wa ukusanyaji wa mapato kabla ya tarehe 30 ya kila mwezi unaofuata baada ya robo mwaka kukamilika kwa lengo la kuongeza ufanisi na kuwezesha utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2023/24; na
 - (xvi) Kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango taarifa za mwenendo wa ukusanyaji wa mapato zilizosuluhishwa kwa kila mwezi, robo, nusu na mwaka pamoja na taarifa za tathmini ya mapato kila robo mwaka. Taarifa hizo ziainishe sababu za kufikiwa/kutofikiwa kwa malengo, changamoto zilizopo na mikakati ya kuhakikisha malengo ya makusanyo yanafikiwa.

1.5. Kiwango cha Ubadilishaji Fedha

92. Makadirio yote ambayo yanatumia fedha za kigeni, yatumie kiwango elekezi cha ubadilishaji fedha za kigeni cha Dola Moja ya Marekani kwa Shilingi za Tanzania 2,345.1 katika kuandaa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2023/24.

1.6. Maandalizi ya Bajeti ya Mishahara

93. Wakati wa kuandaa ikama na bajeti ya mishahara kwa Mwaka 2023/24, Maafisa Masuuli wanaelekezwa yafuatayo:

- (i) Kutoajiri watumishi wapya hadi kuthibitisha upungufu uliopo na iwapo kuna waliozidi wahamishiwe sehemu zenye upungufu ili kuhakikisha uwepo wa msawazo wa watumishi (Manning Level);
- (ii) Kutenga bajeti ya upandishaji vyeo, ajira mpya, ubadilishaji kada/kazi, nafasi za kuhamia na uteuzi kwa kuzingatia Mwongozo wa Katibu Mkuu (OR-MUUB) kuhusu uandaaji wa ikama na makadirio ya bajeti ya mishahara kwa Mwaka 2023/24;
- (iii) Kujumuisha nyongeza ya mwaka ya mishahara (annual increment) katika bajeti ya mishahara kwa mwaka 2023/24 kulingana na ukomo wa bajeti uliopo;
- (iv) Kuhakikisha kila mtumishi anachangiwa katika Mfuko wa Pansheni na Hifadhi ya Jamii kwa kiwango sahihi kinachotakiwa kwa mujibu wa sheria ili kuepuka tozo inayotakana na ucheleweshaji wa mchango; na
- (v) Kuandaa bajeti ya mishahara kwa kuzingatia Waraka wa Watumishi wa Serikali Na. 3 wa Mwaka 2022 na Nyaraka za Msajili wa Hazina Na. 3, 4, 5, 6, 7, 8 na 9 za Mwaka 2022 kuhusu Marekebisho ya Mishahara kwa watumishi wa Umma na Taasisi za Serikali.

1.7. Maandalizi ya Bajeti ya uendeshaji wa Ofisi

94. Wakati wa kuandaa bajeti ya matumizi mengineyo kwa mwaka 2023/24, Maafisa Masuuli wanaelekezwa yafuatayo:

- (i) Kutenga bajeti kwa ajili ya kuwezesha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali kwa kutumia ukomo wa bajeti wa Fungu husika;
- (ii) Kutenga bajeti kwa ajili ya kulipa madeni yaliyozalishwa, hususan madeni yatokanayo na huduma za uendeshaji wa ofisi (posho za kujikimu, stahili za viongozi, likizo, shajala)
- (iii) Kutenga bajeti na kulipa gharama za uendeshaji wa ofisi ikiwemo umeme, maji, simu, mtandao, pango, ulinzi, usafi, mafuta na matengenezo ya magari. Aidha, madeni yatakayozalishwa katika kasma hizi yatalipwa kwa kutumia fedha za matumizi mengineyo za Fungu husika;
- (iv) Kutenga bajeti na kulipa stahili za kisheria kwa watumishi ili kuepuka ulimbikizaji wa madeni, riba na faini;
- (v) Kuzingatia Waraka wa Watumishi wa Umma Na. 1 na 2 wa Mwaka 2022 na Waraka wa Msajili wa Hazina Na. 1 na 2 wa mwaka 2022 kuhusu posho ya kujikimu kwa safari za kikazi ndani ya nchi na posho ya kazi za muda wa ziada;
- (vi) Kutenga bajeti kwa ajili ya mafunzo ya watumishi ikiwemo matumizi ya mifumo mbalimbali ya Serikali;
- (vii) Kutenga bajeti kwa ajili ya kuendelea kuimarisha Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani kwa kuwapatia vitendea kazi na kuwajengea uwezo wa kitaaluma watumishi ili kuongeza mawanda ya ukaguzi (ukaguzi wa fedha na ufanisi);
- (viii) Kuzingatia vifungu sahihi wakati wa uandaaji wa bajeti; na
- (ix) Taasisi na Mashirika ya Umma ambayo hayajaanza kutumia Mfumo mpya wa Usimamizi wa Taarifa za Rasilimali watu na mishahara kutenga bajeti kwa ajili ya maandalizi ya msingi ya kuingia katika Mfumo huu ikijumuisha mafunzo, na uhuishaji wa miundo ya maendeleo ya utumishi ili kuendana na mahitaji ya mfumo.

1.8. Maandalizi na Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo

95. Maafisa Masuuli wanaelekezwa yafuatayo:

- (i) Kuhakikisha kuwa miradi inayoendelea kutekelezwa inapewa kipaumbele kwa kutengewa bajeti ili kuikamilisha kabla ya kuanza miradi mipya;
- (ii) Wizara za Kisekta ambazo zinaratibu miradi na programu zinazoshirikisha utekelezaji wa Mafungu mengine kuhakikisha bajeti zake zinawasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango ili zitengwe kwenye Mafungu husika;
- (iii) Kuzingatia Mwongozo wa Uandaaji Miradi na Majadiliano ya Mikopo, Dhamana na Upokeaji wa Misaada wa mwaka 2020;
- (iv) Kuzingatia Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), SURA 148 na kanuni zake kuhusu Utaratibu wa Kutoa Msamaha wa VAT kwa Miradi inayotekelezwa kwa Fedha za Serikali na za Washirika wa Maendeleo;

- (v) Kuhakikisha misamaha ya kodi inayotolewa katika miradi ya maendeleo inatumika ipasavyo ili kudhibiti matumizi mabaya ya misamaha hiyo;
- (vi) Kuzingatia Waraka wa Hazina Na. 5 wa mwaka 2020/21 kuhusu Mfumo wa Kitaifa wa Kusimamia Miradi ya Maendeleo ((National Projects Management Information System - NPMIS);
- (vii) Kuzingatia Kifungu cha 29(3) cha Sheria ya Bajeti, SURA 439 na Kanuni ya 21(1-3) ya Kanuni za Sheria ya Bajeti za Mwaka (Marekebisho yake ya Mwaka 2021), kinachoelekeza kuhusu uombaji wa idhini ya kuvuka mwaka na fedha kwa mwaka unaofuata ifikapo tarehe 30 Juni kila mwaka; na
- (viii) Kutenga bajeti ya kuandaa miradi inayoweza kutekelezewa kwa utaratibu wa ubia baina ya sekta ya umma na binafsi (PPP). Miradi ya PPP ipewe msisitizo zaidi ili kupunguza utegemezi wa bajeti ya Serikali katika kutekeleza miradi ya maendeleo. Serikali inaendelea kukamilisha taratibu za mapitio ya Sheria ya PPP ili kuifanya wezeshi katika utekelezaji wa miradi kwa njia ya PPP.

1.8.1 Miradi ya Kimkakati ya Kuongeza Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa

96. Katika mwaka 2023/24, Serikali itaendelea kusimamia utekelezaji na ukamilishaji wa miradi ya kimkakati. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kutenga bajeti ya ukamilishaji wa miradi ili kufikia malengo tarajiwa kwa kuzingatia thamani ya fedha.

1.8.2 Ugharamiaji wa Miradi Kupitia Fedha za Nje

97. Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo itaendelea kutekeleza na kugharamia programu na miradi ya maendeleo kwa kuzingatia Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, SURA 134 na Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo. Hivyo, katika kuandaa bajeti ya miradi inayogharamiwa na fedha za nje, Maafisa Masuuli wanaelekezwa:

- (i) Kutoingia Mikataba ya Makubaliano na Washirika wa Maendeleo ya kupokea misaada na mikopo pasipo idhini ya Waziri mwenye dhamana na masuala ya Fedha kwa mujibu wa Kifungu cha 15(1) cha Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, SURA 134;
- (ii) Kuwasilisha takwimu za ahadi za fedha za nje Wizara ya Fedha na Mipango wiki ya kwanza ya Januari, 2023 ili kukamilisha maandalizi ya ukomo wa bajeti za Mafungu;
- (iii) Kuwasilisha ahadi za miradi itakayotekelezwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi na Mashirika ya Umma kutokana na ufadhili wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali Wizara ya Fedha na Mipango kupitia OR - TAMISEMI na Ofisi ya Msajili wa Hazina, wiki ya kwanza ya Januari 2023; na
- (iv) Kutenga mchango wa Serikali (*counterpart fund*) katika miradi ya maendeleo yenye masharti hayo inayotekelezwa kwa ushirikiano na Washirika wa

Maendeleo katika mwaka husika.

1.8.3 Upangaji na Usimamizi wa Fedha zinazopelekwa moja kwa moja kwenye miradi (D - Fund)

98. Katika usimamizi wa fedha za Misaada au Mikopo zinazotolewa na Washirika wa Maendeleo moja kwa moja katika Mafungu kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo (*D- Fund*), Maafisa Masuuli wanapaswa kuzingatia:

- (i) Matumizi ya Mfumo wa Usimamizi wa Fedha Zinazopelekwa Moja kwa Moja kwenye Miradi (*D - Fund Management Information System*); na
- (ii) Maelekezo ya Waraka wa Hazina Na. 2 wa Mwaka 2019 kuhusu Utaratibu wa Kuomba na Kuhamisha Fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwenda Moja kwa Moja kwenye Miradi ya Maendeleo (*Direct to Project Funds*).

1.8.4 Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi

99. Maafisa Masuuli wanaokusudia kutekeleza miradi kwa utaratibu wa Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Binafsi wanaelekezwa kuzingatia Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, SURA 103 na Kanuni zake za mwaka 2020 na Waraka wa Hazina Na. 7 wa Mwaka 2020/21.

1.9. Masuala Mengine ya Kuzingatiwa katika Uandaaji wa Mpango na Bajeti

1.9.1 Masuala ya Muungano

100. Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala na Taasisi za Umma zinaelekezwa:

- (i) Kuendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kufanya vikao vya ushirikiano baina ya Wizara/Taasisi/ Idara za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mara nne (4) kwa mwaka kwa mujibu wa Mwongozo wa Vikao vya Ushirikiano wa mwaka 2019;
- (ii) Wizara/Taasisi/Idara zenye hoja za Muungano ambazo hazijapatiwa ufumbuzi kuendelea kufanya vikao vya majadiliano kwa lengo la kuharakisha upatikanaji wa ufumbuzi wa hoja hizo; na
- (iii) Taasisi za Muungano kuandaa taarifa za utekelezaji wa Masuala ya Muungano mara mbili kwa mwaka na kuziwasilisha Ofisi ya Makamu wa Rais.

1.9.2 Kinga dhidi ya magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukizwa:

101. Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Afya na Halmashauri kutenga bajeti kwa ajili ya ununuzi wa viudadu ili kutokomeza mazalia ya mbu. Aidha, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuchukua hatua nyingine za kuzuia magonjwa yasiyoambukizwa ikiwemo; kutoa elimu kuhusu lishe, afya ya akili na kufanya mazoezi pamoja na kutenga bajeti kwa ajili ya afua za lishe kupitia *Objective Y* katika mfumo wa CBMS.

1.9.3 Mpango Kazi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara (Blueprint):

102. Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji kwa kutekeleza mipango mbalimbali ikiwemo Mpango Kazi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara. Maafisa Masuuli wanaelekezwa yafuatayo:

- (i) Kurazinisha (harmonise) majukumu ya kitaasisi ikiwemo mabaraza ili kurahisisha utoaji huduma;
- (ii) Kuendelea kujenga na kuimarisha vituo jumuishi vya huduma za uwekezaji na biashara;
- (iii) Kutenga bajeti kwa ajili ya Idara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara katika Sekretariati za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- (iv) Kukamilisha kanuni za udhibiti wa Sekta binafsi ili kuwezesha mazingira bora ya ufanyaji biashara na yenye kuleta ushindani sawa; na
- (v) Kuendelea kutekeleza *Blueprint* kwa kufanya mapitio na kuhuisha sheria mbalimbali ili kuweka misingi mizuri ya kusimamia mazingira bora ya kufanya biashara na uwekezaji nchini. Aidha, matokeo ya tathmini hiyo yataisaidia Serikali katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji.

1.9.4 Programu ya Mabadiliko ya Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma Awamu ya Tatu

103. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kutenga bajeti kwa ajili ya kutekeleza Awamu ya Tatu ya Programu ya Mabadiliko ya Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma (PSRP III, 2021 - 2026) ikiwemo kuwajengea uwezo viongozi na watumishi Serikalini; na kuimarisha usimamizi wa rasilimali watu.

1.9.5 Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili

104. Katika kuendeleza Sekta ya Kilimo nchini, Maafisa Masuuli husika wanaelekezwa kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya kutekeleza maeneo ya vipaumbele vya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II, 2017 - 2028) kwa kushirikisha Mamlaka za Serikali za Mitaa. Maeneo hayo ni:

- (i) Kusimamia matumizi endelevu ya maji na ardhi;
- (ii) Kuimarisha upatikanaji wa masoko na kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi ili kuleta ushindani kwenye soko;
- (iii) Kuweka mazingira wezeshi katika uwekezaji wa kilimo, mifugo na uvuvi pamoja na kuimarisha huduma za ugani, uratibu, ufuatiliaji na tathmini; na
- (iv) Kuongeza tija na faida kwenye uzalishaji katika sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi.

1.9.6 Programu ya Uimarishaji Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

105. Katika kutekeleza Programu ya Uimarishaji Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, OR - TAMISEMI inaelekezwa kuendelea kutenga bajeti ya kuwajengea

uwezo watumishi waliopo katika Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika maeneo yafuatayo:

- (i) Uwekezaji wa kiuchumi kwenye Mikoa na Halmashauri;
- (ii) Ushiriki wa jamii katika uaandaji wa Mipango na utekelezaji;
- (iii) Kuimarisha Utawala bora, Utoaji wa huduma, usimamizi wa Rasilimali watu na Fedha;
- (iv) Kuimarisha ugatuaji wa madaraka pamoja na uratibu wa mahusiano ya Serikali kuu na Mamlaka ya Serikali za Mitaa; na
- (v) Kuimarisha uratibu, ufuatiliaji na tathmini katika shughuli za maendeleo.

1.9.7 Uendelezaji wa Sekta ya Fedha

106. Katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma jumuisi za fedha pamoja na kuongeza ufanisi katika upatikanaji wa rasilimali fedha kwenye shughuli zinazochochea ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini kwa wananchi, Serikali inaendelea kutekeleza sera, sheria, kanuni, miongozo na mikakati mbalimbali ili kujenga mfumo thabiti katika sekta ya fedha. Maafisa Masuuli husika wanaelekezwa kuzingatia Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha (2020/21 - 2029/30) wakati wa maandalizi na utekelezaji wa Mpango na Bajeti wa Fungu husika.

1.9.8 Usimamizi wa Mali za Umma

107. Katika kuimarisha usimamizi wa mali za umma, Maafisa Masuuli wakati wa kuandaa Mpango na Bajeti wanaelekezwa:

- (i) Kuendelea kuzingatia Sheria ya Fedha za Umma, SURA 348; Mwongozo wa Usimamizi wa Mali za Umma wa mwaka 2019; Waraka wa Hazina Na. 2 wa mwaka 2021/22 kuhusu Usimamizi wa Mali za Serikali kwa kutumia Mfumo wa Kielektroniki (GAMIS) na Waraka wa Hazina Na.7 wa Mwaka 2018/19 kuhusu Utaratibu wa Umiliki wa Magari na Mali zinazotumika kwenye Miradi inayogharamiwa na Serikali na Fedha za Washirika wa Maendeleo;
- (ii) Kutenga bajeti kwa ajili ya kupima, kuweka alama na kurasimisha maeneo ya ardhi yanayomilikiwa na Serikali ikijumuisha mashamba, viwanja, shule/vyuo, maeneo ya wazi, vituo vya kutolea huduma za afya na ofisi za taasisi za Umma pamoja na kudhibiti usalama na ulinzi wa mali za umma;
- (iii) Kutenga bajeti kwa ajili ya matengenezo ya mali za Serikali kulingana na Mpango wa Matengenezo wa Mali (Asset Maintenance Plan); na
- (iv) Kuhuisha muda wa uhai wa mali uliobaki (Estimated Remaining Economic Life - EREL) kwa lengo la kuipa thamani na kuiwezesha mali kuendelea kutoa huduma iliyokusudiwa kwenye Taasisi.

1.9.9 Mfumo wa Uhasibu Serikalini (MUSE)

108. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuhakikisha Taasisi zao zinatumia Mfumo wa Uhasibu Serikalini (MUSE) kwa mujibu wa Waraka wa Hazina Na. 5 wa mwaka

2019 kuhusu Uanzishaji na Utumiaji wa Mifumo ya Kieletroniki ya Usimamizi wa Fedha za Umma.

1.9.10 Ulipaji na Udhhibiti wa Uzalishaji na Ulimbikizaji wa Madeni

109. Katika kudhibiti uzalishaji na ulimbikizaji wa madeni Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia maelekezo ya Kifungu cha 52(2) cha kikamilifu na kusimamia Mkakati wa Kudhibiti Madeni kwa:

- (i) Kuzingatia Waraka wa Hazina Na. 4 wa Mwaka 2014/15, Waraka wa Hazina Na.1 wa Mwaka 2018/19 na Waraka wa Hazina Na. 3 wa Mwaka 2019 kuhusu Uzuiaji, Udhhibiti na Ulipaji wa Madeni ya Serikali; na
- (ii) Kuhakikisha Hati za Madai zinazotakiwa kulipwa ndani ya siku 28, maombi ya fedha yanawasilishwa Hazina siku 16 kabla. Aidha, kwa Hati za Madai zinazotakiwa kulipwa ndani ya siku 56 maombi yawasilishwe Hazina siku 28 kabla.

1.9.11 Hatua za Kudhibiti Matumizi

110. Serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kusimamia nidhamu ya matumizi ya fedha za Umma ili kuongeza tija na kupata thamani ya fedha. Hivyo, Maafisa Masuuli wanaelekezwa:

- (i) Kutenga bajeti kwa ajili ya kugharamia majukumu ya msingi ya Mafungu kwa kuwa maombi ya nje ya bajeti hayatafanyiwa kazi;
- (ii) Kuzingatia Sheria ya Bajeti, SURA 439 na Sheria ya Fedha za Umma, SURA 348 pamoja na Kanuni zake katika usimamizi wa fedha za umma;
- (iii) Kuzingatia Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 pamoja na Kanuni zake kwa kufanya ununuzi wa pamoja na kutumia Mwongozo wa Matumizi ya *Force Account* wa Mei, 2020 ili kupata thamani halisi ya fedha;
- (iv) Kutumia Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Misamaha ya Kodi ulioanza kutumika tarehe 1 Julai, 2022 kwa ajili ya kuchambua maombi ya Misamaha ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT);
- (v) Kuimarisha uwajibikaji na udhibiti katika usimamizi wa malipo ya mishahara ili kuhakikisha kuwa watumishi wanaolipwa mishahara ni wale wanaostahili na kwa viwango wanavyostahiki;
- (vi) Kutoingia mikataba bila kuwa na bajeti ili kuepuka malimbikizo ya madai kwa kuzingatia Mwongozo Kuhusu Maombi na Utoaji wa Fedha za Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali;
- (vii) Kuendelea na utaratibu wa kutumia Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini (GPSA) kwenye ununuzi wa magari baada ya kupata ushauri wa kiufundi kutoka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Ujenzi) na kibali cha ununuzi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Mfumo wa Kielektroniki wa Utoaji Vibali (GPSA Intergrated Management Information System - GIMIS);

- (viii) Kutumia Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma (TANePS) katika ununuzi wa bidhaa, huduma na kandarasi za ujenzi;
- (ix) Kuongeza matumizi ya TEHAMA katika shughuli za Serikali na kuwajengea uwezo wataalam wa ndani katika usimamizi wa mifumo ili kupunguza gharama;
- (x) Kuzingatia Waraka wa Hazina Na. 5 wa Mwaka 2019 kuhusu Uanzishaji na Utumiaji wa Mifumo ya Kielektroniki ya Usimamizi wa Fedha za Umma katika ununuzi, uandaaji na usimikaji wa mifumo ya kielektroniki ya usimamizi wa fedha za Umma ili kuondoa urudufu wa mifumo;
- (xi) Kuzingatia Waraka wa Rais Na. 1 wa mwaka 1998 kuhusu Hatua za Kubana Matumizi ya Serikali ikiwemo Kudhibiti Ununuzi na Matumizi ya Magari kwa Viongozi katika Utumishi wa Umma;
- (xii) Kuzingatia Waraka wa Mkuu wa Utumishi wa Umma Na.2 wa mwaka 2021 kuhusu utaratibu wa kutumia magari, aina na stahili za magari kwa viongozi katika utumishi wa umma na hii ijitokeze kwenye bajeti ya mafungu husika. Watumishi waliofikia stahiki ya kuendeshwa kwa magari ya Serikali wakopeshwe magari na sio kununuliwa na Serikali;
- (xiii) Kusimamia upelekaji kwa wakati wa ruzuku za Wakala na Taasisi za Serikali zilizo katika Mafungu wanayosimamia; na
- (xiv) Taasisi zinazojenga miundombinu zizingatie ushirikishwaji wa wadau husika wakati wa upangaji na utekelezaji wa miradi.

1.10. Masuala Mtambuka katika Mpango na Bajeti

111. Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa masuala mtambuka. Maafisa Masuuli wanaelekezwa:

- (i) Kuzingatia Mwongozo wa Huduma kwa Watumishi wa Umma Wenye Ulemavu (2008), pamoja na masuala ya Jinsia, VVU, UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukizwa;
- (ii) Kuzingatia Mwongozo wa Utoaji Elimu kuhusu Tatizo la Dawa za Kulevywa Nchini Toleo la Mwaka 2022 ili kudhibiti matumizi na athari zake kwa vijana;
- (iii) Kuendelea kutekeleza Mpango Kazi wa Kutokomeza Ukatili wa Watoto na Wanawake wa mwaka 2017/18 - 2021/22 pamoja na mkakati wa kutokomeza mauaji ya wazee;
- (iv) Kujenga au kukarabati miundombinu ya majengo ili yawe rafiki kwa Watu Wenye Ulemavu na Wazee;
- (v) Kuzingatia Miongozo mbalimbali ya Udhibiti wa magonjwa ya mlipuko ikiwemo UVIKO - 19 kupitia afua mbalimbali katika jamii bila kuathiri shughuli za kiuchumi;
- (vi) Kutekeleza mkakati wa kukabiliana na changamoto ya lishe duni/utapiamlo nchini kwa kutekeleza Mpango wa Pili Jumuishi wa Taifa wa Utekelezaji wa Masuala ya Lishe (NMNAP - II) wa mwaka 2021/22 - 2025/26;

- (vii) Kuendelea kutekeleza Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira utakaotekelezwa kwa kipindi cha miaka 10 kuanzia mwaka 2022 hadi 2032, Kampeni Kabambe ya Kitaifa ya Usafi na Hifadhi ya Mazingira (Kukuza uelewa kwa jamii), na Mwongozo wa Biashara ya Caboni wa Mwaka 2022. Aidha, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kutenga bajeti kwa ajili ya mazingira kupitia *Objective X* katika mfumo wa CBMS;
- (viii) Kutumia kikamilifu rasilimali za maji zilizopo nchini ili kupanua wigo wa fursa zilizopo kwenye uchumi wa buluu; na
- (ix) Kuendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa pamoja na Mikakati ya Kitaasisi ya Mapambano Dhidi ya Rushwa Nchini.

1.11. Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa

112. Serikali itaendelea kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa kwa kutekeleza makubaliano, itifaki na mikataba iliyoridhiwa katika ushirikiano wa kikanda na kimataifa. Maafisa Masuuli wanaelekezwa:

- (i) Kusimamia utekelezaji wa Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo (DCF) wa mwaka 2017/18 - 2024/25 pamoja na mpango kazi wake;
- (ii) Kuzingatia masuala ya ushirikiano kati ya nchi na nchi, kikanda na kimataifa ikijumuisha Kamisheni ya Umoja wa Afrika (AU), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Mashirika ya Kimataifa pamoja na masuala mengine ya mtangamano;
- (iii) Kuainisha na kutumia fursa zinazopatikana kati ya nchi na nchi, kikanda na kimataifa ili kukuza uwekezaji na kuchochea ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu; na
- (iv) Kuwasilisha makadirio ya michango ya uanachama ya Kikanda na Kimataifa Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya kujumuishwa na kutengewa bajeti kabla ya wiki ya kwanza ya Januari, 2023 pamoja na kufuatilia nyaraka muhimu baada ya malipo.

1.12. Maelekezo Mahsusi kwa Taasisi na Mashirika ya Umma

113. Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina itaendelea kuboresha utendaji na usimamizi wa Taasisi na Mashirika ya Umma ili kuongeza ufanisi na tija kwenye utoaji huduma na michango katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali. Katika kufikia azma hiyo, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kutekeleza yafuatayo:

- (i) Kuhuisha Mipango Mkakati ya Taasisi ili iendane na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26;
- (ii) Kuendelea kutumia mifumo ya kielektroniki ya OTRMIS, MUSE, GePG na PlanRep katika kuhuisha taarifa za Bodi za Wakurugenzi na kuingiza taarifa za fedha, matumizi na uandaaji wa taarifa za kiuhasibu, makusanyo ya mapato na uandaaji wa Mpango na Bajeti mtawalia;
- (iii) Kuzingatia Sheria ya Msajili wa Hazina, Sura 370 kwa kutenga na

- kuwasilisha katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali michango ya asilimia 15 ya mapato ghafi ya Taasisi na asilimia 70 ya ziada ya mapato baada ya kutoa matumizi yaliyoidhinishwa;
- (iv) Kuzingatia Sheria ya Utumishi wa Umma Sura 298 na Maelekezo ya Waraka wa Utumishi wa Umma Namba 1 wa Mwaka 2017 hususan kuhusu mamlaka ya Katibu Mkuu - OR-MUUB kuidhinisha Miundo ya Maendeleo ya Utumishi, mishahara, posho, motisha na marupurupu ya watumishi katika Utumishi wa Umma;
 - (v) Kuhakikisha maombi ya kibali cha kuvuka mwaka na fedha na matumizi yake yanawasilishwa Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti, Sura 439 na maelekezo ya Msajili wa Hazina;
 - (vi) Kuhakikisha maombi ya uhamisho wa vifungu wa ndani ya taasisi (*reallocation within*) yanawasilishwa Ofisi ya Msajili wa Hazina;
 - (vii) Kutumia geresho la kibajeti (*GFS Code 2014*) 28211124 - *Contribution to Consolidated Fund* wakati wa kuingiza takwimu za michango itakayowasilishwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali;
 - (viii) Kuandaa na kuwasilisha Mikakati ya Uwekezaji, Sera ya Gawio (dividend policy) na Mipango ya Biashara katika Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa ajili ya kupata idhini;
 - (ix) Kuhakikisha watumishi wote wanaosafiri nje ya nchi wana vibali vya safari kutoka Mamlaka husika. Aidha, uchambuzi wa kina wa maombi ya safari ufanyike kwa kuzingatia taratibu zote za gharama ya safari za kikazi nje ya nchi na kujiridhisha na tija ya safari husika kabla ya kuwasilisha maombi hayo katika Ofisi ya Msajili wa Hazina;
 - (x) Kuingia Mkataba wa Utendaji Kazi pamoja na kuwasilisha utekelezaji wa Mikataba kila robo mwaka kwa mujibu wa Sheria ya Msajili wa Hazina;
 - (xi) Kuibua vyanzo vipya na kusimamia ukusanyaji wa mapato ya ndani;
 - (xii) Kufanyia kazi taarifa za tathmini zinazofanywa na Ofisi ya Msajili wa Hazina na kuwasilisha utekelezaji wake;
 - (xiii) Kuandaa Mpango wa Tathmini za Utendaji wa Bodi za Wakurugenzi na kuziwasilisha kwenye Mamlaka;
 - (xiv) Kuandaa mpango wa kuzijengea uwezo Bodi za Wakurugenzi na kuutekeleza; na
 - (xv) Kutekeleza Muundo na Mgawanyo wa Majukumu ulioidhinishwa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Taifa kwa kujaza nafasi za Uongozi na kufanya mapitio ya nyaraka nyingine za uendeshaji wa taasisi zinazoweza utekelezaji wa miundo.

1.13. Maelekezo kwa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa

1.13.1. Sekretarieti za Mikoa

114. Sekretarieti za Mikoa zinapaswa kutekeleza masuala yafuatayo:

- (i) Kuendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kugharamia vikao vya Kamati ya Usalama ngazi ya mkoa na wilaya;
- (ii) Kuendelea kutambua maeneo ya mipaka na kuweka alama za mipaka ya Mkoa, Wilaya , Tarafa, na upimaji wa maeneo yanayotegemewa kutekeleza miradi;
- (iii) Kutenga bajeti na kuratibu maandalizi ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2024;
- (iv) Kuzingatia kutenga bajeti kwa ajili ya uendeshaji wa ofisi za Wakuu wa Wilaya na ofisi za Maafisa Tarafa;
- (v) Kutenga bajeti ya ujenzi, ukamilishaji, ukarabati na ununuzi wa vifaa kwa ajili ya ofisi na makazi ya Wakuu wa Mkoa, Makatibu Tawala wa Mkoa na Wilaya, Wakuu wa Wilaya na Maafisa Tarafa;
- (vi) Kufuatilia uibuaji wa vyanzo vipya na ukusanyaji wa mapato ikiwemo Kusimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kubuni na kuimarisha vyanzo vilivyopo, kuandaa maandiko ya miradi kwa kutumia Mwongozo wa Uandaaji wa Miradi ya Kimkakati katika Mamlaka za Serikali za Mitaa wa Mwaka 2021;
- (vii) Kuratibu mazingira wezeshi ya kuhudumia wawekezaji na wafanyabiashara, na kuhuisha Wasifu wa Uwekezaji wa Mkoa, na Kusimamia utekelezaji wa Mwongozo wa *National Multisectoral Local Content Guidelines* wa mwaka 2019 katika shughuli za uwekezaji; na
- (viii) Kutenga bajeti ya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Sekretarieti za Mkoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

1.13.2. Mamlaka za Serikali za Mitaa

115. Katika uandaaji na utekelezaji wa Mpango na Bajeti za Mamlaka za Serikali za Mitaa, Maafisa Masuuli wanapaswa kutekeleza maelekezo yafuatayo:

A. Maelekezo ya Jumla

- (i) Kutenga bajeti ya vikao vya kisheria vya Kamati za Maendeleo za Kata na mikutano ya Vijiji na Mitaa;
- (ii) Kuendelea kuzingatia Mwongozo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo Ulioboreshwa mwaka 2019;
- (iii) Kuhakikisha makadirio ya mapato na matumizi ya vituo vya kutolea huduma pamoja na Vijiji/Mitaa yanaandaliwa na kujumuishwa kwenye Mpango na Bajeti ya Halmashauri;
- (iv) Kutenga bajeti ya maandalizi ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2024;
- (v) Kutenga bajeti kwa ajili ya kutambua maeneo ya mipaka na kuweka alama za mipaka ya Halmashauri, Kata, Vijiji/Mitaa na Vitongoji, maeneo ya hifadhi na upimaji wa maeneo yanayotegemewa kutekelezwa miradi; na
- (vi) Kutenga fedha za ujenzi, ukamilishaji, ukarabati na ununuzi wa samani kwa

ajili ya majengo ya utawala na nyumba za viongozi wa Halmashauri, Ofisi za Kata na Vijiji/Mitaa.

B. Mgawanyo wa Mapato ya Ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa

116. Wakati wa kuandaa makadirio ya mapato ya ndani ya Serikali za Mitaa kwa mwaka 2023/24, Maafisa Masuuli wanaelekezwa:

- (i) Halmashauri zenye mapato yasiyolindwa ya shilingi bilioni tano au zaidi zinaelekezwa kutenga kiasi kisichopungua asilimia 60 kwa ajili ya miradi ya maendeleo zikijumuisha asilimia 10 kwa ajili ya Mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu na asilimia 10 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya barabara zinazosimamiwa na TARURA;
- (ii) Halmashauri zenye mapato yasiyolindwa kati ya Shilingi bilioni mbili na shilingi bilioni tano, zinaelekezwa kutenga kiasi kisichopungua asilimia 40 kwa ajili ya miradi ya maendeleo zikijumuisha asilimia 10 ya Mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu;
- (iii) Halmashauri zenye mapato yasiyolindwa chini ya shilingi bilioni mbili, zinaelekezwa kutenga kiasi kisichopungua asilimia 20 kwa ajili ya miradi ya maendeleo zikijumuisha asilimia 10 ya Mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu;
- (iv) Kutenga kiasi kisichopungua shilingi 200,000 kutoka mapato ya ndani ya Halmashauri kwa ajili ya uendeshaji wa ofisi kwa kila Kijiji/Mtaa kila robo mwaka. Aidha, kwa Halmashauri zinazokusanya mapato chini ya shilingi bilioni moja na milioni mia tano zinaelekezwa kutenga kiasi kisichopungua shilingi 100,000 kwa Kijiji/Mtaa kila robo mwaka; na Kuendelea kutenga shilingi 100,000 kila mwezi kwa ajili ya posho ya madaraka ya watendaji wa kata;
- (v) Kuhakikisha mapato yatokanayo na mazao ya kilimo (asilimia 20), mifugo (asilimia 15) na uvuvi (asilimia 5) yanatengwa na kutumika katika sekta husika kulingana na miongozo iliyopo katika kuboresha sekta hizo ikiwa pamoja na uendelezaji wa mazao ya kimkakati;
- (vi) Kuendelea kuhasibu michango ya wadau na nguvu za wananchi ili kupata thamani halisi ya michango kwenye miradi ya maendeleo; na
- (vii) Kutenga bajeti kwa ajili ya kuendeleza mikakati mbalimbali ya uimarishaji na uongezaji wa mapato ikiwemo kupitia, kurekebisha na kutunga Sheria Ndogo za kuimarisha ukusanyaji wa mapato.

C. Maelekezo kuhusu Sekta za Afya, Elimu, Kilimo, Mifugo, Uvuvi, Ardhi, Biashara, Viwanda, Uwekezaji, Maliasili na Mazingira

117. Wakati wa kuandaa makadirio ya mapato ya ndani ya Serikali za Mitaa kwa mwaka 2023/24, Maafisa Masuuli wanaelekezwa:

- (i) Kuboresha huduma za afya kwa kutoa kipaumbele katika ununuzi wa dawa, vifaa na vifaa tiba; kujenga, kukamilisha na kukarabati vituo vya kutolea

- huduma za afya pamoja na huduma za mama na mtoto ikiwemo huduma za chanjo;
- (ii) Kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu dhana na umuhimu wa bima ya afya ili kufikia lengo la Bima ya Afya kwa Wote;
 - (iii) Kutenga shilingi 1,000 kwa kila mtoto mwenye umri wa chini ya miaka mitano kwa ajili ya huduma za lishe;
 - (iv) Kuandaa na kuwasilisha takwimu zenye uhalisia kwa ajili ya kuwezesha utengaji wa bajeti ya Elimumsingi na Sekondari (Kidato cha V na VI) zikijumuisha idadi ya wanafunzi wa Elimu ya awali, Shule za Msingi na Sekondari, Shule za bweni, Maafisa Elimu Kata pamoja na shule mpya zinazostahili kupatiwa vibali vya usajili ifikapo tarehe 30 Januari, 2023;
 - (v) Kutenga bajeti kwa ajili ujenzi wa madarasa ya shule za msingi na sekondari kulingana na uhitaji;
 - (vi) Kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia katika shule za msingi na sekondari kwa kujenga, kutoa nyenzo za kujifunzia na kufundishia hususan vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalum; kukamilisha na kukarabati miundombinu ya shule, kuwezesha michezo shuleni, kuimarisha masuala ya malezi na makuzi, unasihi, usalama wa mtoto, elimu ya afya na usafi wa mazingira shuleni na nyumbani na kuendelea kuhamasisha jamii kutekeleza mkakati wa upatikanaji wa chakula shuleni;
 - (vii) Kutenga bajeti kwa ajili ya kuimarisha usimamizi wa maendeleo ya Ushirika pamoja na kuweka mifumo itakayoongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wanaushirika;
 - (viii) Kutenga maeneo ya uwekezaji, viwanda na biashara;
 - (ix) Kuwawezesha wajasiriamali wadogo (Wamachinga) kwa kuwapatia elimu ya biashara na ujasiriamali na kuwaunganisha na taasisi za fedha na masoko;
 - (x) Kutenga bajeti kwa ajili ya kulinda na kutunza vyanzo vya maji ikiwa ni pamoja na kuviwekea mipaka;
 - (xi) Kutenga bajeti kwa ajili ya kutoa elimu ya uhamasishaji kwa wakulima, wafugaji na wavuvi kushiriki katika ujenzi wa miundombinu ya kilimo, mifugo na uvuvi kwa kushirikiana na sekta husika;
 - (xii) Kuhuisha Wasifu wa Kiuchumi katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
 - (xiii) Kuendeleza na kupanga mipango miji na matumizi bora ya ardhi hususan miji midogo inayochipukia na kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji na kuzingatia Mwongozo wa Kitaifa wa Uhamasishaji Jamii Ujenzi wa Nyumba Bora wa Mwaka 2019 pamoja na Mwongozo wa Utoaji wa Vibali vya Ujenzi na Usimamizi wa Ujenzi wa Majengo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa wa mwaka 2018;
 - (xiv) Kuendelea na uwekaji wa miundombinu ya anwani za makazi; na
 - (xv) Kutenga bajeti ya usimamizi na uendelezaji wa maliasili na mazingira

ikiwemo: uendelezaji na utangazaji wa vivutio vya utalii, kuhifadhi maeneo oevu, upandaji miti, utunzaji misitu na maeneo ya hifadhi; na kuhakikisha teknolojia za uzalishaji zinazingatia uhifadhi wa mazingira; uzoaji na uondoshaji wa taka.

1.14. Uingizaji wa Takwimu za Bajeti ya Serikali kwenye Mifumo ya CBMS na PlanRep

118. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kukamilisha uingizaji wa takwimu sahihi za bajeti kwenye Mifumo ya *CBMS* na *PlanRep* kwa kuzingatia muda uliopangwa pamoja na masuala muhimu yafuatayo:

- (i) Kusimamia usahihi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa kuzingatia ukomo wa Bajeti kwa mwaka 2023/24 na makisio yanayoonesha uhalisia kulingana na ukomo wa miaka miwili inayofuata (2024/25 - 2025/26);
- (ii) Matumizi sahihi ya namba za miradi zinazotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango, geresho za bajeti (GFS codes 2014) zilizoboreshwa, vizio vya vipimo kama vilivyoainishwa kwenye mifumo ya CBMS na PlanRep na bei za bidhaa kama ilivyoainishwa katika orodha ya Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini (GPSA); na
- (iii) Kutumia mfumo katika kuandaa Mpango Kazi na Mtiririko wa Mahitaji ya Fedha ya shughuli zilizopangwa kwenye bajeti.

1.15. Uwasilishaji na Uchambuzi wa Mpango na Bajeti

119. Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa kuwasilisha Muundo wa Mapato na Matumizi wa Muda wa Kati (MTEF) OR – TAMISEMI; na Taasisi na Mashirika ya Umma kwa Ofisi ya Msajili wa Hazina wiki ya tatu ya Januari, 2023 kwa ajili ya uchambuzi baada ya kuidhinishwa katika vikao vya kisheria.

120. Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara zinazojitegemea na Sekretariati za Mikoa wanatakiwa kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango nakala mango (*hard copy*) mbili (2) ya makadirio ya mapato na matumizi ya Fungu husika, siku tano (5) kabla ya kuanza uchambuzi kwa mujibu wa ratiba itakayotolewa. Aidha, Maafisa Masuuli wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wanaelekezwa kuwasilisha muhtasari wa makadirio ya mapato na matumizi katika nakala mango.

121. Uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi utafanywa na Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na OR – MUUB, OR -TAMISEMI na Ofisi ya Msajili wa Hazina kuanzia wiki ya nne ya mwezi Januari, 2023. Aidha, uchambuzi wa Mpango na Bajeti utazingatia Muundo wa uwasilishaji wa MTEF uliobainishwa katika Sura ya Pili ya Sehemu ya Pili ya Mwongozo. Vile vile, Ofisi ya Msajili wa Hazina inaelekezwa kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango taarifa ya Uchambuzi

wa Mipango na Bajeti za Taasisi na Mashirika ya Umma wiki ya pili ya mwezi Machi, 2023.

122. Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi nyingine za Umma wanatakiwa kuwasilisha nakala tete (*soft copy*) ya MTEF Wizara ya Fedha na Mipango, OR - TAMISEMI na Ofisi ya Msajili wa Hazina zilizofanyiwa marekebisho ndani ya siku tano (5) baada ya bajeti ya Fungu husika kuidhinishwa na Bunge.

1.16. Uwasilishaji wa Randama

123. Maafisa Masuuli wa Mafungu wanaelekezwa kuwasilisha Randama Ofisi ya Waziri Mkuu tarehe 10 Machi, 2023 kwa mujibu wa Kanuni Na. 115(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge (Toleo la Mwaka 2020). Aidha, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuwasilisha Randama kwenye Kamati za Kudumu za Bunge za Kisekta kwa kuzingatia ratiba ya vikao vya kamati husika itakayotolewa na Ofisi ya Bunge. Uwasilishaji wa Randama uzingatie: Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2021/22 na Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2022/23 kwa kipindi kinachoishia Februari, 2023; changamoto na utatuzi wake; maelekezo ya Kamati za Bunge za Kisekta; na Mpango na Bajeti wa Mwaka 2023/24.

1.17. Ufuatiliaji, Tathmini na Utoaji wa Taarifa za Utekelezaji

124. Ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa Mpango na Bajeti utazingatia Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26), Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma wa mwaka 2015 na miongozo mingine iliyopo kwenye sekta mbalimbali.

1.17.1. Ufuatiliaji na Tathmini

125. Katika kuimarisha ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti, Maafisa Masuuli wanaelekezwa:

- (i) Kuzingatia Waraka wa Hazina Namba 5 wa mwaka 2021/22 na Mfumo wa Kitaifa wa Kusimamia Miradi ya Maendeleo (NPMIS);
- (ii) Kutenga bajeti kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti na kuhakikisha inatumika kwenye shughuli husika kama ilivyoidhinishwa na Bunge;
- (iii) Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao kusimamia uhuishaji wa mifumo ya ukusanyaji wa mapato ili kuwezesha mapato yote kukusanywa sehemu moja na kuhakikisha kuwa mifumo yote inafanyiwa ukaguzi maalum kila baada ya nusu mwaka;

- (iv) Shughuli za ufuatiliaji na tathmini kwenye miradi ya maendeleo ziratibiwe na Idara ya Sera na Mipango kwa kushirikiana na idara/vitengo vingine;
- (v) Kutenga bajeti kwa ajili ya kufanya tathmini ya utekelezaji wa sera hususan zilizotekelezwa kwa zaidi ya miaka mitano;
- (vi) Kuhakikisha takwimu za matumizi ya fedha za ndani za makusanyo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na ruzuku kutoka Serikali kuu zinaingizwa kwenye Mfumo wa MUSE ifikapo tarehe ya mwisho ya kila mwezi ili kupata taarifa sahihi za matumizi kwa mwezi husika; na
- (vii) Mkaguzi wa Ndani asimamie uimarishaji wa vikao vya Kamati ya Bajeti kwa ajili ya kupitia na kujadili taarifa za ufuatiliaji, tathmini na utekelezaji kila robo mwaka ili kuleta uwazi na uwajibikaji.

1.17.2. Uwasilishaji wa Taarifa za Utekelezaji

126. Kwa kuzingatia Kifungu Na. 55(4) cha Sheria ya Bajeti, SURA 439 na Kanuni ya 29(5), Maafisa Masuuli wanatakiwa kuandaa na kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango taarifa za utekelezaji za kila robo mwaka pindi inapomalizika. Aidha, taarifa za utekelezaji za robo mwaka na mwaka mzima kutoka Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ziwasilishwe kupitia OR - TAMISEMI na za Taasisi na Mashirika ya Umma ziwasilishwe kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina na nakala kwa Wizara mama.

127. Taarifa za utekelezaji ziandaliwe na kuwasilishwa katika nakala mango na tete kwa kuzingatia muundo ulioainishwa katika Sura ya Pili ya Sehemu ya Pili ya Mwongozo huu. Aidha, Maafisa Masuuli wanatakiwa kuwasilisha nakala tete za taarifa za shughuli za Serikali kupitia Dashibodi ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Taarifa zote ziwasilishwe katika muda wa siku 30 baada ya kukamilika kwa robo ya mwaka husika.

128. Maafisa Masuuli wa Wizara za Kisekta wanaelekezwa kuandaa taarifa na takwimu zitakazowezesha zoezi la tathmini ya mpango na bajeti (Public Expenditure Review) itakayofanyika kila robo mwaka. Zoezi hili litawezesha kubaini kasi ya utekelezaji wa miradi ya kisekta.

SURA YA PILI
MUUNDO WA UANDAAJI NA UWASILISHAJI WA TAARIFA ZA MPANGO
NA BAJETI KWA MWAKA 2023/24

2.1 Utangulizi

130. Sura hii inaainisha muundo na fomu mbalimbali zinazopaswa kuzingatiwa na Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi na Mashirika ya Umma katika hatua za uandaaji, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini pamoja na uwasilishaji wa taarifa za utekelezaji wa mpango na bajeti.

131. Katika kuandaa na kuwasilisha taarifa za Mpango na Bajeti kwa mwaka 2023/24, Maafisa Masuuli wanapaswa kuzingatia maelekezo yaliyopo katika sheria, mpango, mifumo na miongozo ya uandaaji na usimamizi wa bajeti kama ifuatavyo: Sheria ya Bajeti, Sura 439; Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura 134; Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348; Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26); Mwongozo wa Uandaaji wa Mpango Mkakati wa Muda wa Kati na Bajeti (MTSPBM); na Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma (PIM-OM).

132. Mifumo itakayotumika ni pamoja na: Mfumo wa Uandaaji na Usimamizi wa Bajeti (CBMS); Mfumo wa Kielektroniki wa Ukusanyaji Mapato Serikalini (GePG); na Mfumo wa Uhasibu Serikalini (MUSE); Mfumo Shirikishi wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS); Mfumo wa Kitaifa wa Kusimamia Miradi ya Maendeleo (NPMIS); Mfumo wa D - Fund MIS; Mfumo wa Uandaaji wa Mipango na Utoaji wa Taarifa za Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma (PlanRep); Mfumo wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato Serikali za Mitaa (TAUSI); Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato Vituo vya Afya (GoTHoMIS); na Mfumo wa Malipo na Utoaji wa Taarifa za Matumizi ya Fedha Katika Vituo vya Kutolea Huduma (FFARS).

2.2 Maandalizi ya Mpango na Bajeti

133. Katika kuandaa Mpango na Bajeti Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma wanaelekezwa kuzingatia Mfumo wa Muda wa Kati wa Matumizi (MTEF) unaohusisha fomu za makadirio ya mapato na matumizi. Ufafanuzi wa fomu hizo ni kama ifuatavyo:

(a) Makadirio ya Mapato

134. Katika kuandaa na kuwasilisha makadirio ya mapato, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuingiza takwimu sahihi kwenye mifumo ya kibajeti ili kupata taarifa za mapato kwenye **Fomu Na. 4** (Revenue Estimates and Projections) kwa

kutumia geresho la bajeti toleo la 2014 (GFS Codes 2014 Series) zilizo sahihi.

(b) Makadirio ya Matumizi

135. Katika kuandaa na kuwasilisha makadirio ya matumizi, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia yafuatayo:

- (i) **Matumizi ya Kawaida:** Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuingiza takwimu sahihi kwenye mifumo ya kibajeti ili kupata taarifa za matumizi ya mishahara katika Fomu Na. 8A - 8F na Fomu Na. 9. Aidha, wanaelekezwa kuingiza takwimu sahihi ili kupata taarifa za matumizi mengineyo katika **Fomu Na. 3A - 3C.**
- (ii) **Matumizi ya Maendeleo:** Katika kuandaa makadirio ya matumizi ya maendeleo, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuingiza takwimu sahihi kwenye mifumo ya kibajeti ili kupata taarifa za matumizi ya maendeleo katika **Fomu Na. 6, 6.1, 10A na 10C.**
- (iii) **Uandaaji wa Vigezo vya Kupima Matokeo:** Katika kuandaa viashiria vya kufikia malengo na shabaha za Taasisi, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuingiza taarifa za viashiria na takwimu ili kupata taarifa za matokeo katika **Fomu Na. 7.**
- (iv) **Makadirio ya Ajira zitakazozalishwa:** Katika kuandaa makadirio ya ajira mpya zitakazozalishwa kutokana na utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo, Maafisa Masuuli wanapaswa kujaza kikamilifu **Fomu Na. 15A** na kuwasilisha Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira, na Wenye Ulemavu.

2.3 Mpangokazi na Mtiririko wa Mahitaji ya Fedha

136. Kabla ya kuanza utekelezaji wa bajeti iliyoidhinishwa na Bunge, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuingiza takwimu sahihi kwenye mifumo ya kibajeti ili kupata mpangokazi na mtiririko wa mahitaji ya fedha katika **Fomu Na. 11A (R), 11A (D), 11B (R), 11B (D), 14B (R) na 14B (D).**

2.4 Taarifa za Utekelezaji wa Mpango na Bajeti

137. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuandaa na kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa mpango na bajeti za robo mwaka na mwaka mzima kwa kujaza kikamilifu **Fomu Na. 5, 6.2, 12A, 12B, 12C, 13A na 13B** na kuziwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango. Aidha, Fomu Na. 15B inapaswa kujazwa na kuwasilishwa Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira, na Wenye Ulemavu. Vile vile, Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wanatakiwa kuingiza takwimu sahihi kwenye mfumo wa PlanRep ili kupata taarifa za utekelezaji wa Mpango na Bajeti katika **Fomu Na. 13C1, 13C2, 13C3, 13C4 na 13C5** na kuziwasilisha OR - TAMISEMI kupitia Mfumo wa PlanRep.

MUUNDO WA UWASILISHAJI WA MTEF 2023/24 - 2025/26

Maelezo ya Kisera kwa Ufupi

- (i) Maelezo ya Waziri/Mkuu wa Mkoa/Meya au Mwenyekiti wa Halmashauri/Mwenyekiti wa Bodi/Baraza
- (ii) Maelezo ya Afisa Masuuli.

Sura ya 1: Uchambuzi wa Hali Iliyopo

- 1.1 Uchambuzi wa Wadau
- 1.2 Uchambuzi wa Uwezo, Udhaifu, Fursa na Changamoto
- 1.3 Masuala Muhimu ikijumuisha mawasilisho ya usimamizi wa vihatarishi

Sura ya 2: Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti

- 2.1 Mapitio ya Utekelezaji - 2021/22
 - 2.1.1 Muhtasari wa Fedha zilizovuka mwaka kwa kila programu na maelezo ya matumizi 2021/22
 - 2.1.2 Makadirio ya Mapato kwa Mwaka yakilinganishwa na Mapato Halisi
 - 2.1.3 Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka yakilinganishwa na Matumizi Halisi
 - 2.1.4 Muhtasari wa Malengo yaliyopangwa yakilinganishwa na Malengo yaliyofikiwa
- 2.2 Mapitio ya Utekelezaji kwa Nusu Mwaka - 2022/23
 - 2.2.1 Muhtasari wa Fedha zilizovuka mwaka kwa kila programu na maelezo ya matumizi 2022/23
 - 2.2.2 Makadirio ya Mapato kwa Mwaka yakilinganishwa na Mapato Halisi
 - 2.2.3 Makadirio ya Matumizi ya Mwaka yakilinganishwa na Matumizi Halisi
 - 2.2.4 Muhtasari wa Malengo kwenye MTEF yakilinganishwa na Mafanikio yaliyopatikana
- 2.3 Changamoto zilizojitokeza 2021/22 na Mikakati ya kukabiliana na changamoto

Sura ya 3: Makadirio ya MTEF (2023/24 - 2025/26)

- 3.1 Muhtasari wa Makadirio ya Bajeti ya Mwaka na Miaka Miwili inayofuata (Fomu Na.1)
- 3.2 Malengo Makuu, Shabaha na Shughuli zitakazofanyika (Fomu Na. 3A)
- 3.3 Makadirio ya Matumizi ya Mengineyo kwa Mwaka na Miaka Miwili inayofuata (Fomu Na. 3B)
- 3.4 Muhtasari wa Makadirio ya Matumizi ya Kawaida (Fomu Na. 3C)
- 3.5 Makadirio na Maoteo ya Mapato (Fomu Na.4)
- 3.6 Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo kwa Mwaka na Miaka Miwili inayofuata (Fomu Na.6)
- 3.7 Muhtasari wa Matumizi ya Miradi ya Maendeleo (Fomu Na. 6.1)
- 3.8 Mfumo wa Matokeo wa Kitaasisi (Fomu Na.7)
- 3.9 Muhtasari wa Makadirio ya Mishahara kwa kila Fungu (Fomu Na. 8A)
- 3.10 Muhtasari wa Makadirio ya Mishahara kwa Kifungu (Fomu Na. 8B)
